# Nipashe

Jumatatu Mei 4, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580222

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mwigulu waziri wizara 3 miaka mitano ya JPM

UK. 2




UKURASA 11

## MAAJABU MAABARA YA CORONA

# Vipimo papai, mbuzi vyaonyesha 'positive'



**JPM** aagiza ichunguzwe, asema atatuma ndege kufuata dawa ya corona Madagascar, asisitiza walimu kuendelea kulipwa mishahara, atoa msimamo uzikaji ...*Endelea ukurasa 2*

Rais John Magufuli akizungumza jana, baada ya kumwapisha Dk. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Hafla hiyo ilifanyika wilayani Chato mkoani Geita. **PICHA: IKULU**.

## BAA LA CORONA



Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), visa vilivyoripotiwa hadi Mei 2, vya maambukizo ya Covid 19 ni 3,267,184, vifo 229,971.

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## UKAGUZI WABAINI UFISADI MABILIONI YA PRIDE

UKURASA 9

## RIPOTI MAALUM

# Waziri: Corona imesababisha majanga mazao manne nchini

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store


**MICHEZO** MAGUFULI: NAFIKIRIA KURUHUSU LIGI KUU UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Mwakilishi wa wazee wa kabila la Wahehe mkoani Iringa, Gerald Malangalila, akiwa ameshika bunduki yake, baada ya kufyatua risasi mbili kati ya tisa zilizopangwa kufyatuliwa wakati wa maziko ya aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustino Mahiga, juzi, katika makaburi ya Tosamaganga mkoani Iringa kabla ya kuzuiliwa na vyombo vya usalama. **PICHA: FRANCIS GODWIN**.

# JPM ashangaa 'madudu'

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameshangazwa na kinachoonekana maajabu katika Maabara Kuu ya Taifa baada ya kutoa majibu ya sampuli za mimea na wanyama, zikidaiwa zina virusi vya corona.

Amesema hatua hiyo inatokana na uchunguzi wa siri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto dhidi ya utendaji wa chombo hicho, baada ya kukitilia shaka.

Katika hotuba yake jana mjini Chato mkoani Geita baada ya kumwapisha Waziri mpya wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, Rais aliorodhesha sampuli saba, ikiwa ni baadhi ya walizoziwasilisha katika maabara hiyo.

Alizitaja kuwa ni za wanyama, mimea na kemikali kama vile kondoo, ndege aina ya kware, papai, fenesi, sungura, oili ya magari, ambazo walizipa majina batili ya binadamu na zikarejeshewa majibu ya uchunguzi, yanayokanganya wa ukweli wa kisayansi.

"Nimemshukuru sana Katibu Mkuu mpya, Profesa (Mabele) Mchembe, wameenda na kufanya 'mambo'. Tulichukua sampuli za mbuzi, kondoo, papai, mafuta ya gari na vitu vingine mbalimbali tukavipeleka pale maabara bila wao kujua na tukavipa majina," alisema.

Aliendelea: "Oil tuliipa jina la Jabir Hamza (30), majibu yalitoka 'negative' (hakuna athari). Tunda aina ya fenesi tulilipa jina la Sarah Samwel (45), majibu yalikuwa 'unconclusive' (haiko bayana).

"Papai tulilipa jina la Elizabeth Ame (26), majibu yalikuja 'positive' (kuna athari), ndege aina ya kware majibu yalikuja 'positive', sungura majibu yalikuja 'positive', mbuzi majibu yalikuja 'positive', kondoo majibu yalikuja 'negative'.

"Sasa, kama tulipeleka sampuli ya fenesi ambayo tuliipa jina la Sarah Samweli (45), nayo mafenesi yalitakiwa yapelekwe 'isolation'? Kwa hiyo, ukishagundua kitu hiki, lazima ujue kuna mchezo wa ajabu unafanyika.

"Sasa, ukishaona umepeleka sampuli, ukamwambia huyu ni binadamu halafu ukaletewa 'positive', sasa maana yake mapapai yote nayo yale yangewekwa 'isolation'.

"Zile sampuli zinatoka nje, kwa hiyo lazima kuna kitu fulani kinafanywa kama mapapai yanaonekana yana corona. Basi WHO (Shirika la Afya Duniani) inabidi ifanye kazi kubwa katika hili. Na kama mbuzi nao wana corona, basi wanasayansi hatujafanya ya kutosha katika hili."

Kutokana na hilo, Rais Magufuli ambaye ni mbobezi katika taaluma ya Kemia, alimwagiza Waziri Mwigulu kushirikiana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kufanya uchunguzi kwenye maabara hiyo ili kuibua uhalisia unaoendelea.

Alieleza hofu yake kwamba kuna uwezekano wa ama taaluma isiyojitokesheleza kwa baadhi ya watendaji wa maabara hiyo, au kutumiwa na wasiokitakia mema chombo hicho nyeti kwa usalama wa umma.

"Pia, waziri nimekuapisha leo (jana), itabidi mkafanye uchunguzi wa masuala fulani ya hii maabara ya kitaifa ya Tanzania, iliyokuwa inahusika kupima corona. Kuna 'controversial' (utata) nyingi ambazo ni za ajabu, walikuwa wanatoa matokeo tu kwamba ni 'positive' mara nyingi," alisema.

Vilevile, Rais aliwaondoa hofu Watanzania kuhusu maradhi hayo, kwamba kuna uwezekano wa watu kuishi wakaishi nayo kama baadhi ya magonjwa kama Ukimwi, kifua kikuu na surua, huku wakiendelea na matibabu na hakuna haja ya kutishana.

Katika hatua nyingine, Rais alikemea kauli za kisiasa zisizo na tija katika vita hivyo dhidi ya corona, baadhi wakitaka kufungwa kwa baadhi ya miji na huduma zake muhimu kama vile masoko.

"Mtu anazungumza funga Dar es Salaam, funga Tanga. Sifungi nilishasema! Ni lazima Watanzania tuishi, tuchape kazi na tuendelee kuchukua tahadhari. Mwingine anasema 'funga masoko'. Hivi nikifunga Soko la Kariakoo, unadhani watu watakula nini?" Rais Magufuli alihoji kwa mshangao.

"Nitoe wito kwa Watanzania, msiwe na hofu. Kwanini uwe na hofu? Mbona mafua yamekuwapo lakini haya ni mafua 'advanced' (ya ngazi ya juu) yatapita. Lazima kuna watu wameambiwa ni wagonjwa na wengine wakafa kwa hofu," alihitimisha.

# ... asisitiza walimu kulipwa mishahara

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amesema licha ya shule kufungwa kwa muda usiojulikana kutokana na tishio la virusi vya corona, serikali itaendelea kuwalipa mishahara walimu na wafanyakazi wengine.

Alitoa kauli hiyo jana mjini Chato mkoani Geita, alipomwapisha Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba.

Machi 17 mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitangaza kufungwa kwa shule na vyuo kwa muda usiojulikana ili kudhibiti kusambaa kwa virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu.

"Mimi 'nime-experience' katika miezi miwili mitatu iliyopita ya ugonjwa huu, nchi yetu ina waajiriwa wengi kama walimu, asilimia karibu 49 ya waajiriwa wote ni walimu, lakini tumeendelea kulipa mishahara bila hata wao kufundisha. Nchi nyingi zimeshindwa.

"Ninataka kuwathibitishia walimu, tutaendelea kuwalipa mishahara yenu mpaka shule zitakapofunguliwa, na wafanyakazi wengine tutaendelea kuwalipa mishahara mpaka mambo mengine yakae sawa na hiyo ndiyo maana halisi ya kutoumiza uchumi kwa sababu hili tatizo litaondoka," alisema.

Rais Magufuli pia alizungumzia dawa ya corona, akieleza kuwa amewasiliana na Rais wa Madagascar kuhusu kuipata dawa hiyo ili Watanzania wanaougua waitumie.

"Nimewasiliana na watu wa Madagascar kuna dawa kule ya corona wanasema wameipata. Nitatuma ndege hiyo dawa ije hapa tuitumie. Wengine wanasema nipo Chato, hapa si ndipo nilipozaliwa na hata nikifa, nitazikwa hapa. Kuna ubaya gani nikiwa Chato? Tuache siasa za ajabu," alisema.

Rais pia aliwataka Watanzania kuacha tabia ya kuzusha taarifa za vifo kwamba kila anayefariki dunia, anafariki kwa ugonjwa wa corona.

"Siku hizi hata mtu akijiua ndani kwake, polisi wakija kuchukua mwili wanasema corona. Ikitokea ajali polisi wamefika kuchukua miili napo corona.

"Watanzania corona isitutishe, inawezekana kuna watu wengine wamekufa kwa sababu ya hofu tu. Viongozi wa dini msitupotoshe, nampongeza Mufti amesema sisi tutaendelea kufunga wakati wote wa Mfungo wa Ramadhani. Watanzania tusimame imara tumeshashinda hii vita.

"Wengine wako Dar es Salaam wanasema watu wasiende bungeni, na nimeagiza wasilipwe posho maana utalipwa kwa kazi uliyofanya, kuna mambo ya ajabu yanafanyika," alisema.

Rais Magufuli pia alieleza kusikitishwa na uamuzi wa kuuzika mkoani Mtwara mwili wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mtwara badala ya kuusafirisha kwenda kuzikwa nyumbani kwao Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Mkuu wa Mkoa wa Mtwara nikamwona siku moja anazungumza kwamba 'Mkuu huyu wa Wilaya amefariki, hatuwezi kusafirisha atazikwa hapahapa.'' Ilinisikitisha sana, walishindwaje viongozi wa Mtwara kumsafirisha DC akaenda kuzikwa kwa heshima kule kwao Moshi?

"Kama madakrari waliweza kuvaa PPE (vifaa/mavazi ya kujikinga na maambukizo) wakati wanamtibu, kwanini alipofariki (dunia) wasimvalishe hayo mavazi na kuufunga mwili vizuri kisha wakausafirisha?" Rais Magufuli alihoji.

## Mwigulu wizara tatu miaka 5

**Na Salome Kitomari,**

DODOMA

WAHENGA walisema "usikate tamaa ungali unaishi". Ndicho kinaonekana kwa Waziri mpya wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba.

Amekuwa waziri wa pili kutumbuliwa na Rais John Magufuli kisha kurejeshwa, akiungana na mawaziri wengine wawili waliohudumu katika wizara tatu tofauti tangu serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani Novemba 5, 2015.

Mawaziri wengine waliohudumu wizara tatu katika uongozi wa Rais John Magufuli Angella Kairuki na George Simbachawene, ambaye alikuwa wa kwanza kurejeshwa baada ya kutumbuliwa. Mawaziri hawa wamepitia Wizara ya Mambo ya Ndani Nchi, na walipotolewa waliendelea kuwa wabunge kwa mujibu wa Katiba.

Safari ya uwaziri Dk. Mwigulu ilianza Desemba 10 mwaka 2015 alivyoteuliwa kuwa waziri wa iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, lakini Juni 2016 alihamishiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na nafasi yake kuchukuliwa na Dk. Charles Tizeba, Rais alipomtema Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwanga, katika baraza lake.

Julai 2018, Dk. Mwigulu aliondolewa kwenye nafasi hiyo kwa kile kilicholezwa na Rais kuwa alishindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo, na nafasi yake kupewa Kangi Lugola, ambaye aliondolewa mapema mwaka huu.

Safari ya uwaziri wa Simbachawene ilianza 2015 alipoteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kisha kuondoka kwenye baraza Septemba 2017 baada ya kuandika barua kwa Rais Magufuli barua ya kujiuzulu baada ya kutajwa katika ripoti za uchunguzi wa mwenendo wa madini ya tanzanite na almasi. Hata hivyo, Julai mwaka jana, Rais Magufuli alimteua kuwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), akichukua nafasi ya Januari Makamba.

Kairuki aliingia kwenye baraza hilo mwaka 2015 akiwa Waziri anayeshughulikia Utumishi na Utawala Bora, lakini baadaye alihamishiwa Wizara mpya ya Madini.

Januari mwaka jana, Kairuki aliondolewa na kupelekwa kuanzisha Wizara mpya ya Uwekezaji, huku naibu wake katika Wizara ya Madini, Doto Biteko, akipandishwa kuwa waziri kamili.

## HABARI KITAIFA

# Tabora yapewa barakoa za mil. 20/-

**Na Tiganya VincenT,** TABORA

KAMPUNI ya Usafirishaji ya Athwal (ATT) ya mjini Tabora, imetoa msaada wa barakoa zenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa uongozi wa Mkoa wa Tabora.

Msaada huo ulikabidhiwa jana na Ofisa Usafirishaji wa ATT, Godfrey Tarimo, kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, ili kuunga mkono juhudi za serikali za kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19.

Alisema kampuni hiyo ambayo inatoa huduma za usafirishaji ndani na nje ya Tabora, imeamua kutoa msaada huo ili kusaidia katika mapambano dhidi ya virusi vya corona mkoani Tabora.

Akipokea msaada huo, Mwanri, alisema umekuja wakati muhimu ambapo Taifa liko katika vita ya kudhibiti ugonjwa wa Covid-19 usiendelee kusambaa.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema wadau wote mkoani humo wanapaswa kuungana katika vita ili hatimaye waweze kuushinda ugonjwa wa Covid-19.

Alisema msaada huo walioupokea baada ya kuthibitishwa na wataalamu wa sekta ya afya kuwa ni za viwango, na kwamba zitagawanywa katika wilaya zote za mkoa huo kwa ajili ya kuwasaidia watoa huduma za afya, ambao wanasaidia kukabiliana na virusi hivyo pamoja watu wengine ambao hawana uwezo wa kuzinunua.

Mwanri alitoa wito kwa wadau wengine wanaoendesha shughuli zao, zikiwamo za biashara kuendelea kushirikiana na serikali katika mapambano dhidi ya corona.

Katika hatua nyingine, Mwanri ameagiza maeneo yote yanayotoa huduma kama sokoni na stendi kufungwa vipasa sauti ili watu wanaofanyia kazi maeneo hayo waendelea kupata elimu ya kujikinga na Covid -19.

Hatua hiyo inalenga kuhakikisha wasafiri na wafanyabiashara wanaokuwapo katika maeneo hayo wanapata elimu sahihi ya kukabiliana na kujikinga virusi vya corona.

Mwanri alitoa agizo hilo alipokutana na viongozi wa masoko, stendi na wajane wakati akiongoza timu ya wataalamu wa afya kutoa elimu ya kujikinga na Covid -19.



Mchimbaji mdogo kutoka mgodi wa Ntambalale Namba Nane, Boke Waitete, jana, akinawa mikono kabla ya kuingia shimoni kuendelea na shughuli yake ya uchimbaji wa madini kama moja ya mbinu ya kupambana na virusi vya corona. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Waziri aagiza msako mitungi 15,000 kukabili baa la corona

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ameliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria watu ambao watabainika kumiliki mitungi ya kuhifadhi Oxygen ya Kampuni ya Tanzania Oxygen Limited.

Amesema mitungi hiyo inatakiwa irudishwe kiwandani ili itumike kujaza gesi kwa ajili ya wagonjwa waliolazwa hospitalini baada ya kuambukizwa virusi vya corona.

Bashungwa alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipotembelea kiwanda hicho kwa lengo la kuona hatua zinazochukuliwa kuhakikisha gesi kwa ajili ya matumizi ya hospitali inapatikana ili kupambana na corona.

"Sasa hivi tunapambana na huu ugonjwa, hiyo mitungi ni muhimu sana kwani wagonjwa wanaihitaji kwenye hospitali. Kwa hiyo, Jeshi la Polisi lifanye kazi yake ili mitungi hiyo irudi, iokoe maisha ya watu," aliagiza.

Mkurugenzi wa Masoko wa Kiwanda hicho, Daudi Mlwale, alisema zaidi ya mitungi 15,000 ipo nje ya mzunguko licha ya kampuni kutoa matangazo kwa kina kutaka irejeshwe bado mwitikio ni mdogo.

Alisema kuna haja ya kila mtu kutambua kuwa ugonjwa wa corona ni vita, hivyo kusiwapo na mtu anahujumu mpango wa usambazaji gesi katika hospitali kwa kuwa gesi hiyo ni muhimu sana kwa wagonjwa.

Aliongeza kuwa kampuni hiyo tayari imeshatoa namba za simu ambazo mmiliki atapiga kutoa taarifa na kampuni itafuata mitungi hiyo popote ilipo.

Virusi vya corona (Covid-19) viligundulikwa kwa mara ya kwanza China Desemba mwaka jana na tayari vimesababisha vifo vya zaidi ya watu 200,000 katika mataifa na maeneo ya utawala 185 duniani.

# Waingiwa hofu mafuriko kaya 106 zikikosa makazi

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI

KAYA 106 zenye watu zaidi ya 400 katika Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, hazina mahala pa kuishi baada ya nyumba zao kujaa maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Kutokana na tatizo hilo, wananchi hao wamepewa hifadhi katika Shule za Msingi S.K. na Omundongo zilizoko katika wilaya hiyo, hadi makazi yao yatakapokuwa salama.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi walioathiriwa na mafuriko hayo akiwamo Lucia Mkagaruki, walisema walizingirwa na maji na wakashindwa kuvuka hadi askari wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji walipokwenda kuwaokoa na kuwapeleka eneo salama.

"Askari walipofika, wakawa wanatuita tuvuke, hatukuweza maana maji yalishakuwa mengi, walilazimika kuja kutuvusha na watoto wetu tukapelekwa ng'ambo ya pili, lakini mali zetu zote zilibaki huko, wasingeweza kutuvusha sisi na mizigo yetu," Lucia alisimulia.

Mwathirika mwingine wa mafuriko hayo, Erica Johnbosco, alisema wanashukuru kwa kuokolewa na kupewa hifadhi na serikali, lakini hofu yake ni kutokuwa na chakula pale mvua itakapokwisha na wao kurejea katika makazi yao.

"Mazao yote yameharibika, tulikuwa na migomba, mihogo, viazi, magimbi na mengine, lakini yote yamemezwa na maji, hatujui tutakula nini tukirejea nyumbani," alisema.

Naye Johnbosco Benedicto alisema kuwa baada ya kupewa hifadhi katika shule, kila chumba kimoja cha darasa zinakaa familia nne na kuwa wanalala kwa kuchanganyikana na watoto wao.

"Wataalamu wa afya kutoka halmashauri walikuja wakatupa elimu namna gani tujikinge na ugonjwa wa corona, tumepewa ndoo na sabuni, tunanawa ili kuhakikisha tupo salama," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

**TAARIFA KWA UMMA**

Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe **09/05/2020** kampuni ya chico (china henan international cooperation group co.ltd ) itasafirisha mzigo (Machine EPROIC D45 Driller) wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TABORA kuelekea DODOMA kupitia ITIGI**, gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM/ 509BKM** ,yenye escort no T643 CVZ

Gari hilo linavipimo vifuatavyo
- Urefu mita 20.00m
- Upana 3.00m
- Kimo 4.5m

**Njia itakayo tumika ni TABORA hadi DODOMA kupitia ITIGI**

Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa **12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu**

157277

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

**TAARIFA KWA UMMA**

Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe 04/05/2020 kampuni ya chico (china henan international cooperation group co.ltd) itasafirisha mzigo (Machine EPROIC D45 Driller) wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DODOMA kuelekea TABORA kupitia ITIGI** , gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM/ 509BKM** ,yenye escort no T643 CVZ

Gari hilo linavipimo vifuatavyo
- Urefu mita 20.00m
- Upana 3.00m
- Kimo 4.5m

Njia itakayo tumika ni **DODOMA hadi TABORA kupitia ITIGI**

Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion

**Tunaomba radhi kwa usumbufu**

DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUNUNUA VITENGE

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 04.05.2020 HADI TAREHE 12.05.2020 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255627428470 au barua pepe jean.kabore@drc.ngo**

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA TAREHE 14.05.2020 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.**

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@drc.ngo AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI KIBONDO VINGINEVYO NI BATILI.**

# Waziri: Corona imesababisha majanga mazao manne nchini

**Na Sanula Athanas,** ALIYEKUWA DODOMA

- Chai hali mbaya, mengine yanafuata
- Adokeza umakini hifadhi ya chakula



WIZARA ya Kilimo imesema mlipuko wa virusi vya corona, umesababisha madhara makubwa kwa chai nchini, zao lililoingizia nchi fedha za kigeni wastani wa Sh. bilioni 100 kwa msimu uliopita wa kilimo.

Akizungumza na Nipashe jijini Dodoma wiki iliyopita, Waziri mwenye dhamana na kilimo, Japhet Hasunga, alisema mbali na chai inayoongoza kwa hali mbaya, mengine yaliyo katika mkumbo wenye mwelekeo huo ni kahawa, tumbaku na pamba.

Hasunga (pichani), alifafanua kuwa eneo kuu la athari linahusu kushuka kwa bei ya mazao ya biashara yanayosafirishwa nje, huku chai ikiwa katika hali mbaya zaidi.

Kwa mujibu wa waziri huyo, sababu kuu ya athari hiyo inatokana na taifa jirani la Kenya ambako ndiko kwenye soko jijini Nairobi, kufunga mipaka yake kutokana na janga la corona, huku Tanzania ikipategemea zaidi.

"Chai ndiyo tumeathirika kabisa kwa sababu minada ya Kenya imefungwa. Tanzania tulikuwa hatuna mnada wa chai, sasa ndiyo tunapambana kuanzisha mnada wa chai," Hasunga alibainisha.

Pia, alisema athari katika mazao mengine yaliyobaki, kwamba licha ya kutofikia athari zilizojitokeza kwa chai, nayo yameshuka bei na kuziingiza katika hatihati ya ufanisi wa kimasoko kwa kiwango kikubwa.

"Kwenye upande wa 'exports' (mauzo ya nje ya nchi), mazao yetu karibu yote tuliyokuwa tunayauza nje yanaonekana kushuka bei. Kwa mfano, pamba imeshuka bei kwa kiwango kikubwa.

"Kahawa pia tunatarajia itashuka kidogo. Itashuka bei kwa sababu walaji wakubwa, zile 'movements' zao zitakuwa 'restricted' (zitazuiwa). Utakuta baadhi ya maeneo wamefunga kabisa vile vioski vya kahawa, hiyo ina maana kwamba bei ya kahawa inaweza ikaathirika kwa kiwango fulani," alisema, huku akidokeza dalili ya athari hizo kwa tumbaku.

Mbali na athari za mauzo ya nje ya nchi, Hasunga pia alitaja sura ya pili iko katika kupanda kwa bei ya mbolea na viuatilifu, inayoendana na dalili za tishio la njaa, hivyo akawataka wananchi kujihami kwa kuhifadhi chakula.

Baadhi ya maeneo maarufu yanakozalishwa mazao yaliyotajwa na Waziri Hasunga ni Tukuyu, Mufindi, Lushoto, Amani - Muheza (Chai); Tabora, Shinyanga, Kigoma (tumbaku); Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Mara (pamba), Bukoba, Moshi, Tukuyu, Mbozi, Mbinga, Lushoto (kahawa).

Ripoti ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), inabainisha kuwa, chai iliyozalishwa na kuuzwa nje ilikuwa tani 29,243.841 kwa mwaka 2018/2019, na kuiingizia nchi Dola za Marekani 43,890,138 (Sh. bilioni 100.906).

Kwa mujibu wa CAG, Charles Kichere, mwaka mmoja kabla, nchi iliuza tani 29,160.642 zilizoingiza Dola za Marekani 62,167,167 (Sh. bilioni 142.925).

Ifuatayo ni sehemu ya ufafanuzi wa Waziri Hasunga, alipohojiwa na Nipashe:

**SWALI: Mlipuko wa virusi vya corona umeathiri vipi sekta ya kilimo hasa katika 'import na export'?**

**HASUNGA:** Kwanza kabisa, mlipuko wa hii homa ya mapafu ijulikanayo kama COVID-19, umeathiri kwa kiwango kikubwa kwenye upande wa 'imports' (bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi).

Sisi tunategemea sana kuagiza mbolea kutoka nje, tunaagiza pia dawa kutoka nje, yaani viuatilifu, lakini tumekuwa tunaagiza mbegu. Sisi imetuathiri sana kwenye upande wetu kwa sababu bei zimepanda, na uzalishaji kule kwenye soko la dunia umeshuka.

Kwa hiyo, tunatarajі kwamba baadhi ya mbolea bei zikapanda zaidi kuliko ilivyo sasa hivi. Ndiyo maana tumetumia hii nafasi katika mkakati ambao tunaufanya, tumeagiza kampuni kuhakikisha zinaagiza mbolea za kutosha kipindi hiki.

La sivyo, itafikia kipindi kama hatujaagiza, tukawa na upungufu. Kwa hiyo, hili tunataka tukabiliane nalo kwa kuagiza mapema. Na nina uhakika tayari mfumo wetu wa BPS watakuwa wanaufungua hivi karibuni. Kwa hiyo, hili eneo tumeathirika kwa kiwango fulani.

Pia kuna vifungashio ambavyo tulikuwa tunaagiza kutoka nje, tunatarajia bei yake huenda isiwe nzuri sana.

Kwenye upande wa 'exports' (bidhaa zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi), mazao yetu karibu yote tuliyokuwa tunayauza nje yanaonekana kushuka bei. Kwa mfano, pamba imeshuka bei kwa kiwango kikubwa.

Kahawa pia tunatarajia itashuka kidogo, itashuka bei kwa sababu walaji wakubwa, zile 'movements' zitakuwa 'restricted' (zitazuiwa), utakuta baadhi ya maeneo wamefunga kabisa vile vioski vya kahawa, hiyo ina maana kwamba bei ya kahawa inaweza ikaathirika kwa kiwango fulani.

Tumbaku pia tumepata hiyo shida. Kwenye chai ndiyo tumeathirika kabisa kwa sababu minada ya Kenya imefungwa. Tanzania tulikuwa hatuna mnada wa chai, sasa ndiyo tunapambana kuanzisha mnada wa chai.

Kwa hiyo, ina maana moja kwa moja unakuta tumeathirika kwa kiwango kikubwa sana. Minada ya mazao kama mbogamboga, matunda, maua imeathirika kwa kiwango fulani.

Kwa njia nyingine, baadhi ya mazao imekuwa kama fursa, kama mazao ya chakula. Imekuwa ni fursa kwa sababu nchi nyingi zimefunga mipaka, lakini wanahitaji chakula. Imekuwa ni fursa kwa sababu usafiri ukipatikana, tunaweza kwenda kuuza na kuuza kwa bei nzuri.

Ni fursa pia kwa Watanzania kuongeza uzalishaji, ni fursa ya kuuza baadhi ya vyakula, lakini yale ya kibiashara yataathirika kidogo na kushuka kwa bei, machache sana ambayo bei inaweza ikabaki palepale au kuongezeka.

**SWALI: Serikali imejipangaje kuhakikisha wananchi wana uhakika wa kupata chakula katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na baa la corona?**

**HASUNGA:** Kwanza, tunawahamasisha wananchi wenyewe watunze chakula ili kwamba wanapovuna, wahifadhi vizuri. Na sasa hivi sisi tatizo la chakula si kubwa kama nilivyosema awali.

Tunachojipanga sisi ni kuhakikisha kwamba, kama tutafikia mahali tutazuia watu kutoka majumbani, tutawezaje kusafirisha chakula kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Hiyo ndiyo itakuwa changamoto yetu kubwa.

Kwa hiyo, sasa hivi tumeagiza maeneo yote; sisi kama nchi tumeigawa katika kanda nane na kila kanda tunahakikisha kunakuwa na akiba na maghala ya chakula. Maghala yapo ya kutosha, ya mpunga yapo ya kutosha, ya mahindi nayo yapo ya kutosha, vijijini huko yapo yamejaa.

Tunataka vyakula vyote vihifadhiwe katika maeneo yale, lakini pia sehemu zinazohitajika, zitumike. Kikubwa zaidi tunachokitaka sisi ni kwamba, sasa tuko kwenye mkakati wa kuagiza dawa kwa ajili ya kuhifadhi mahindi ili yasiharibike, lazima yapate dawa, yaani viuatilifu vilivyo sahihi kwa ajili ya kutunza yasibunguliwe na wadudu. Hili nalo tumejipanga.

Kubwa zaidi ambalo tunataka lifanyike kwenye upande wa chakula ni kwamba, chakula ambacho tunakitegemea kama taifa, tathmini inaonesha tunaweza kupata zaidi ya tani milioni 20 za nafaka na mazao mengine.

Kwa hiyo, tuna imani uzalishaji ni mkubwa ambao haujawahi kutokea katika historia ya nchi yetu. Chakula tunacho kingi, hatuna shida.

Mwishoni mwa mwaka jana, virusi vya corona vilitambuliwa kwa mara ya kwanza mjini Wuhan, China. Hadi jana saa sita mchana, zaidi ya watu milioni 2.97 walikuwa wameripotiwa kuambukizwa virusi hivyo katika nchi 185, huku zaidi ya watu 206,000 wakipoteza maisha kutokana na ugonjwa huo na zaidi ya 868,000 wamepona.

Mlipuko wa virusi hivyo tayari umeonekana kuwa na madhara karibu kwa sekta zote, uchukuzi (usafiri wa anga) na utalii zikiwa zimeathirika zaidi katika maeneo yote duniani kutokana na uamuzi wa nchi nyingi kufunga mipaka.

***USIKOSE KESHO UFAFANUZI WA WAZIRI HUYO KUHUSU MUSTAKABALI WA KILIMO NA CHAKULA NCHINI**

HABARI KITAIFA

# Rufani matibabu ya ughaibuni zapungua

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

SERIKALI imesema rufani za watu kwenda nje ya nchi kutibiwa, zimepungua kutoka 385 mwaka 2015/16 hadi 53 mwaka 2019/20 kutokana na kuimarishwa kwa huduma za matibabu ya kibingwa nchini.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo bungeni mwishoni mwa wiki, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema wizara imeendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa nchini, ili kuokoa maisha ya wananchi wengi sambamba na kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufani ya matibabu nje ya nchi.

"Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Hospitali za Rufani za Kanda na Taifa ziliwasilisha wizarani idadi ya wagonjwa 92 waliokuwa na mahitaji ya kupatiwa matibabu nje ya nchi. Kati yao, 53 walipatiwa kibali cha kwenda kutibiwa nje ya nchi kulinganisha na rufani 554 mwaka 2015/16, ambapo wagonjwa 385 walipatiwa kibali na kwenda kutibiwa nje ya nchi," alibainisha.

Waziri huyo pia alisema katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, wizara kupitia hospitali ngazi ya taifa na kanda imehudumia jumla ya wagonjwa 1,763,950. Kati yao, wagonjwa wa nje walikuwa 1,613,841 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 150,109 ikilingalinishwa na wagonjwa 1,388,286 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2018/19.

Alisema kati ya hao wagonjwa wa nje walikuwa 1,160,243 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 247,979 kati yake wagonjwa hao 1,763,950 waliohudumiwa katika hospitali hizo, jumla ya wagonjwa 304,735 walikuwa ni wagonjwa wa misamaha, na walizigharimu hospitali hizo za rufani za taifa na kanda jumla ya Sh. 31,430,076,324.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, ilihudumia jumla ya wagonjwa 428,700, na kwamba wagonjwa wa misamaha walikuwa 121,136 ambao waliigharimu hospitali kiasi cha Sh. 15,267,868,594 katika kipindi hicho.

KUPANDIKIZA FIGO

Alisema katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya wagonjwa 13 walipata huduma ya upandikizaji wa figo na kwamba jumla ya wagonjwa 56 tangu huduma hizo zilipoanza kutolewa mwaka 2018 walipatiwa huduma.

"Hospitali imetumia jumla ya Sh. bilioni 1.68 kwa wagonjwa 56 ikiwa ni wastani wa Sh. milioni 30 kwa mgonjwa mmoja. Wagonjwa hao wangepatiwa matibabu hayo nje ya nchi, wangeigharimu serikali jumla ya Sh. bilioni 6.72 kwa gharama ya Sh. milioni 120 kwa mgonjwa mmoja," alisema.

Ummy alisema serikali imeokoa jumla ya Sh. bilioni 5.04 na kwamba hospitali imeweka lengo la kufanya upandikizaji wa figo kwa wagonjwa watano kila mwezi.

VIFAA VYA USIKIVU

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, upandikizaji vifaa vya usikivu kwa watoto umefanyika kwa wagonjwa 30 tangu huduma hiyo ianze kutolewa mwaka 2017 na zimetumika Sh. bilioni 1.08 kwa gharama ya Sh. milioni 36 kwa mgonjwa.

Alisema kuwa kama wagonjwa hao wangepatiwa matibabu nje ya nchi, ingegharimu kiasi cha Sh. bilioni tatu kwa gharama ya Sh. milioni 100 kwa kila mgonjwa, hivyo serikali imeokoa kiasi cha Sh. bilioni 1.92.

Aliongeza kuwa jumla ya wagonjwa 288 walipata huduma ya kuruhusu upasuaji wa shingo na kichwa, kuondoa uvimbe kwenye sehemu ya kinywa, uso na shingo, kuweka mirija kwenye figo, kuzibua mirija ya nyongo iliyoziba, kuzibua mirija ya uzazi na kuondoa usaha ndani ya tumbo.

Ummy alisema wagonjwa 846 wamehudumiwa na kwa Sh. bilioni 6.78 (Sh. milioni nane kwa mgonjwa) kulinganishwa na gharama ya Sh. milioni 98 kwa mgonjwa na kama angepata huduma nje ya nchi, hivyo kuiwezesha serikali kuokoa Sh. bilioni 76.14.

Mbali na uimarishaji wa huduma za matibabu ya kibingwa nchini, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2018/19, inabainisha kuwa rufani za matibabu ya Watanzania nje ya nchi zimepungua kutokana na Hospitali za Rufani za Apollo, India kukataa kupokea wagonjwa wanaotibiwa kwa mkopo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF sasa izimulike upya kanuni za ligi

**HATIMAYE** jana Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilikaa ili kujadili hatima ya Ligi Kuu Bara ikwa ni kuitika wito wa Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), ambalo linataka hadi ifikapo Mei 5, mwaka huu kujua hatima ya Ligi Kuu za wanachama wake.

Kutokana na janga la virusi vya corona (COVID-19), mapema wiki iliyopita Caf iliwaandikia wanachama wake TFF ikiwa miongoni mwao, ikitaka kujua hatima ya Ligi Kuu za mashirikisho yote kama itaendelea ama kufutwa ili kuweza kupanga kalenda ya michuano yake.

Hatua hiyo, ndiyo iliyosababisha TFF kuamua kujifungia jana ili kuweza kutoka na jibu moja la ama ligi hiyo itaendelea au la na kama itafutwa ni timu zipi zitakazoiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Caf; Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Ingawa bado haijajulikana TFF itakuja na hatima gani kuhusu kuendelea ama kuufuta msimu huu wa 2019/20, kwa namna hali ilivyo tunaona itakuwa ni vigumu ligi hiyo kuendelea kwa sasa kutokana na ukweli kwamba Machi 17, mwaka huu wakati serikali inasitisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ikiwamo michezo kulikuwa na mtu mmoja pekee aliyebainika kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona tofauti na hali ilivyo kwa sasa.

Hadi kufikia jana mchana jumla ya watu 480 walishabainika kukutwa na maambukizo ya virusi vya corona, huku 16 wakipoteza maisha na 167 wakipona kutoka katika idadi hiyo, hivyo ni dhahiri maambukizi yameongezeka zaidi jambo linaloweza kusababisha TFF kuja na maamuzi ya kushtua, ingawa jana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli alisema anafikiria kwa siku zijazo kutoa ruhusu ya ligi hiyo kuendelea.

Hata hivyo, wakati Rais Magufuli akiendelea kulitafakari hili ikiwa ni pamoja na kupokea ushauri kutoka kwa wataalamu wake, huku TFF na Bodi ya Ligi (TPLB) ikijifungia kujadili, tunalitaka shirikisho hilo na wanachama wake kuketi mapema ili kumulika upya kanuni za ligi hiyo kwa kufanya marekebisho kwa baadhi ya vipengele kabla ya msimu mpya kuanza.

Kipengele muhimu ambacho kinapaswa kuingizwa katika kanuni za ligi hiyo ni cha hatima ya bingwa na timu zitakazoshuka na kupanda daraja endapo patatokea ligi kutokumalizika kwa namna yoyote ile kama ambavyo inaelekea kuwa hivyo msimu huu kutokana na janga hili la corona linaloitesa dunia ambapo hadi jana alasiri jumla ya watu 3,503,311 duniani kote walishathibitika kupatwa na maambukizi, vifo vikiwa ni 245,151 na waliotibiwa na kupona 1,128,958.

Tunatambua huu ni wakati mgumu zaidi kwa TFF na TPLB kuweza kufanya maamuzi kuhusu hatima ya timu zitakazoshuka daraja na zitakazopanda, lakini pia timu itakayoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika ambalo, mwakilishi huwa ni bingwa wa Kombe la Shirikisho maarufu FA Cup.

Kwa maoni ya wengi ikiwamo klabu shiririki za Ligi Kuu Bara, kila moja inaonekana kuwa roho kwatu kwa kuruhusu Simba kutawazwa bingwa wa Ligi Kuu na kuwa mwakilishi wa nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, hasa kwa kuzingatia pointi zake 71 kileleni huku ikiwa mbele kwa tofauti ya alama 17 wakati huu ligi hiyo ikiwa imebakiza mechi 10 kabla ya kufikia ukingoni.

Lakini suala la timu zipi zishuke daraja na zipi zipande pamoja na mwakilishi wa nchi kwenye Kombe la Shirikisho bado ni utata mkubwa kwa TFF, hivyo, janga hili la corona linapaswa kuwa chanzo cha mabadiliko kwa kila kipengele ambacho kinaweza kujakuleta utata wa maamuzi yoyote endapo ligi ikishindwa kumalizika.

Tumeona namna ambavyo imekuwa rahisi kwa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, na ile ya Uholanzi, Eredivisie kufutwa msimu huu na moja kwa moja kufahamika mabingwa ambao watawakilisha mataifa hayo kwenye michuano ya kimataifa na hatima ya zilizopaswa kushuka na kupanda Ligi Kuu kutokana na kuwapo kwa kanuni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Magufuli ameirahisisishia kazi TFF na Bodi ya Ligi



Na Adam Fungamwango

**JANA** Bodi ya Ligi ilitarajiwa kukaa kwa ajili ya kujua mustakabali wa michezo ya soka nchini, ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Michuano hiyo na mingine ya mpira wa miguu, ilisimama Machi 17, mwaka huu kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19 ambao unasababishwa na virusi vya corona, uliosambaa duniani kote.

Ligi nyingi duniani zimesimama, huku baadhi ya nchi zikichukua misimamo yao kama vile kutangaza mabingwa, kufuta ligi, huku zingine zikifikiria kuendelea kuanzia mwezi huu na kuendelea.

Hivi karibuni hapa nchini kumekuwa na mhemko kwa baadhi ya wadau wa soka kuitaka Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka nchini kukaa na kutoa msimamo wake kutokana na janga hili kuonekana bado lipo nchini.

Na hii ni baada ya kusikia nchini Kenya, klabu ya Gor Mahia imepewa ubingwa, huku nchini Ufaransa klabu ya PSG nayo ikapewa ubingwa kwa sababu shughuli za kijamii, huenda zikaendelea kama kawaida mwezi Septemba.

Baada ya hali hiyo ikawa sasa kama shinikizo, baadhi wakiitaka Bodi ya Ligi kutangaza bingwa wa Tanzania ambaye moja kwa moja ingekuwa klabu ya Simba inayoongoza kwa pointi 71.

Mijadala ikawa mikali kweli kweli, wengine wakikataa bingwa asitangazwe, badala yake ligi ifutwe kabisa, msimu huu kusiwe na mshindi wala bingwa.

Kuna waliopendezwa kuwa ifutwe, lakini bingwa wa msimu uliopita wa ligi ambayo ni Simba na bingwa wa Kombe la FA ambayo ni Azam FC ziteuliwe kwenda kucheza michuano ya kimataifa.

Hata hivyo, wapo walioona huko juu wala hakuna tatizo, ila chini kwa timu zinazoshuka daraja, lakini pia zinazotarajiwa kupanda.

Wapo waliopendekeza timu nne za chini zishuke moja kwa moja daraja, lakini baadhi wakapendekeza msimu huu zisishuke hata timu moja na timu zilizotakiwa kupanda zisipande.

Vyovyote itakavyokuwa, ni lazima maamuzi yoyote yangeumiza baadhi ya timu na kuzinufaisha zingine.

Faraja kwa wanamichezo imeanza kurejea baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kusema kuwa anafikiria kurejesha ligi zote za Tanzania.

Akizungumza na wananchi, pamoja na mambo mengine, Rais aliwataka Watanzania waendelee kuchapa kazi na wasiwe na hofu.

"Watanzania tusiwe na hofu, tuendelee kuchapa kazi, wanasiasa waache kutumia hii kama ajenda, haitaweza kuwasaidia, Watanzania lazima tuishi, kwa siku zinazoendelea ninafikiri kuruhusu hata ligi za mipira ziendelee, nasubiri wataalamu wangu wanishauri," alisema.

Kwa kauli hii inaonyesha mwangaza kuwa Ligi ya Tanzania sasa inaweza kuendelea na yale mawazo kuwa ingefutwa, au timu kutangazwa bingwa kabla haijamalizika sasa halipo.

Sidhani sasa kama ulikuwapo mpango wa kufuta ligi au kumpa mtu ubingwa utakuwapo tena. Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi yake ya Ligi (TPLB) baada ya kauli ya Rais, wanachotakiwa kufanya sasa ni angalau kuruhusu timu kuanza mazoezi, lakini tahadhari zikichukuliwe, wakisubiri kauli nyingine na si mpaka itoke ruhusa ndiyo ligi ianze haraka haraka.

Wachezaji kufanya mazoezi kama alivyosema rais ni tiba tosha, kwa sababu ni kweli hatujasikia kesi yoyote ya mchezaji mwenye corona.

Wakati huu wa corona inahitajika si wachezaji tu, lakini hata watu wa kawaida wafanye mazoezi.

Tunachosubiri sasa kusikia baada ya hapo ni utaratibu mzima au mpango mkakati wa TFF na bodi yake ya ligi, kama vile baadhi ya nchi zinazofikiria kurejesha ligi ikiwamo England kutangaza klabu kurejea mazoezini, lakini ituambie kama ikirejea itachezwa kwa mtindo ule ule wa nyumbani na ugenini, au kuna viwanja viteuliwa kwa ajili ya mechi zilizosalia, ili mradi tu kuziwekea mazingira klabu zijue nini zinatakiwa kufanya.

## HABARI KITAIFA

# Wakuu wa shule wajadili namna kusaidia wanafunzi wenye mitihani

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WALIMU wakuu wa shule za msingi Wilaya ya Wete kisiwani Pemba, wamekutana kupanga mikakati na kujadili njia za kuwasaidia wanafunzi hususan wanaojindaa na mitihani yao ya Taifa wakati huu wa ugonjwa wa COVID 19, ili kuendelea kulinda vipaji vyao.

Baadhi walisema pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuanzisha utaratibu wa kuwafundisha wanafunzi kwa njia ya redio na runinga na kuwanufaisha zaidi wanafunzi, lakini kuna changamoto.

Maulid Ali Salim, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mkote, alisema changamoto hiyo inatokana na usikivu wa vituo vya redio na runinga vya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kuwa sio wa uhakika.

"Ni vyema serikali ya wilaya ikaiangalia hili kwa jicho la ziada kwani itakuja kuleta athari kwa wanafunzi hasa wanaojindaa na mitihani," alisema.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Bopwe, Ali Makame Ali, alisema maeneo ya vijiji baadhi ya familia ni maskini, hawana uwezo wa kumiliki TV , hivyo inawawia vigumu kufuatilia masomo.

"Changamoto ya kukatika katika matangazo ya ZBC inasababisha wanafunzi kukata tamaa ya kuendelea kufuatilia, hivyo tunaomba serikali kuu ifahamu changamoto hiyo," alieleza.

Maryam Mbarak Nassor, Mwalimu Mkuu Shule ya Mitiulaya, alisema wanafunzi wengi hawana mwamko wa kufuatilia runinga na kutazama redio, hivyo zinahitajika juhudi za ziada kuwasimamia kuangatia na kusikiliza vipindi.

"Juzi niliwaambia wanafunzi kufuatilia vipindi kwenye redio, walinijibu kwamba kwenye TV hatufahamu, iweje kwenye redio," alifahamisha.

Mkurugenzi wa Baraza la Mji, Suleiman Juma Pandu na Katibu Tawala Wilaya hiyo, Mkufu Faki Ali, waliwashauri kuanzisha utaratibu wa kuandaa maswali na kuwapatia wanafunzi ikiwa ni njia ya kuwafanya waendelee kujisomea.

"Nashauri utaratibu huu usimamiwe na wajumbe wa kamati za shule, mwalimu unaandaa maswali na kumpatia mjumbe wa kamati kuyafikisha kwa wanafunzi , na wakati wa kurejesha majibu iwe ni vivyo hivyo," alishauri Mkufu.

Mkuu wa Wilaya ya Wete, Kepteni Khatib Khamis Mwadini, alisema msaada na maamuzi kutoka serikali kuu unahitajika juu ya suala hilo.

"Hii ni changamoto ambayo nitaiwasilisha serikali kuu ili tuone tunawasaidiaje vipi wanafunzi wetu," alisema.

Hata hivyo, walimu hao walikubaliana kuandaa maswali na kuwapelekea wanafunzi majumbani kupitia wajumbe wa kamati za shule.



Wasichana waliokimbia ukeketaji ambao sasa wanalelewa katika kituo cha Nyumba Salama Butiama mkoani Mara, wakishona barakoa wanazotumia kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA**

ANASTAZIA POLI MARKO AMBAYE NI MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU RASHID ABDALLAH DACHI MKAZI WA SHINYANGA.

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YA KIWANJA **NAMBA 888** NA **890 KITALU "CC"** MATANDA MANISPAA YA SHINYANGA, AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2014 MAENEO YA MATANDA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA ANASTAZIA POLI MARKO KWA **SIMU NAMBA 0767-722115**
**RB NAMBA SHY/RB/2020**

# Shehena ya kwanza yawasili Bandari ya Kwala

**Na Elizabeth Zaya**

SHEHENA ya kwanza ya kontena 29, imewasili katika Bandari Kavu ya Kwala iliyoko Kibaha mkoani Pwani kwa njia ya treni kutoka Bandari ya Dar es Salaam.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, akizungumza katika hafla ya upokeaji wa treni hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki bandarini huko, alisema hiyo ni mara ya kwanza kwa bandari hiyo kupokea kontena ikiwa ni kiashiria cha kuanza rasmi kwa bandari hiyo iliyojengwa ili kusaidia kupunguza mrundikano wa mizigo kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema kuanza kwa shughuli hizo kumefanikiwa baada ya kukamilika sehemu ya mradi huo ambao jumla ya hekta 5.5 zimewekwa zege na reli kwa ajili ya kupokea kontena.

Alisema eneo hilo ambalo ni sehemu ya hekta 60 zinazotarajiwa kujengwa, litakuwa na uwezo wa kuhifadhi kontena 500 kwa wakati mmoja.

Nditiye alisema msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam umekuwa ukisababisha malalamiko kutoka kwa wateja na kuishukuru serikali ya awamu ya tano pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kwa kusimamia mradi huo hadi kufikia hatua ya kuanza kupokea shehena.

"Bandari hii inafungua ukurasa mpya na mwanzo wa operesheni za kuondoa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, kazi ambayo pia itapunguza kuingia kwa malori ya mizigo katikati ya jiji na hivyo kupunguza foleni za magari na kulinda miundombinu ya barabara zetu," alipongeza.

Nditiye alisema amefarijika kuona kazi kubwa iliyofanyika ikiwamo ujenzi wa sakafu ngumu katika eneo hilo kwa ajili ya kuhudumia makasha, ujenzi wa mitaro ya kuzuia mafutiko, miundombinu ya awali ya umeme, maji, Tehama, ulinzi, zimamoto, nyumba za watumishi na ofisi.

Aliiagiza Bodi na Menejimenti ya TPA kuhakikisha bandari hiyo inatumika vizuri na kukamilisha ujenzi kwa kuzingatia vigezo vyote vya ubora.

Alisema uongozi wa Wilaya ya Kibaha na Mkoa wa Pwani unapaswa kuutumia uwapo wa bandari hiyo kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa mkoa huo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TPA, Profesa Ignas Rubaratuka, alisema mradi huo ni matokeo ya dhamira ya dhati ya serikali ya awamu ya tano ya kupunguza msongamano ndani na nje ya Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema mradi huo ni utekelezaji wa dhana ya 'Hapa Kazi Tu' uliyoanza kufuatia maelekezo ya serikali baada ya kuona eneo hilo linafaa zaidi kuliko lile la Kisarawe.

Profesa Rubataruka alitoa wito kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya Tanzania kutumia bandari zilizopo kwa kuwa utendaji na usalama umeimarika zaidi.

"Tumeweza kurudisha heshima ya bandari kwa kuongeza ufanisi na kuimarisha usalama na bado tunaendelea na kuboresha bandari za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara ili kuongeza ufanisi zaidi na kuvutia wateja wapya na kurudisha wale wa zamani ambao walituhama," aliahidi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MATUMIZI SAHIHI YA NAMBA ZA SIMU**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inaendelea kuwakumbusha wananchi na wadau wote wa Mawasiliano kuzingatia matumizi sahihi ya namba za mawasiliano ya simu kulingana na matumizi yake kama yalivyoidhinishwa na TCRA kwa kuzingatia mpango wa kitaifa wa namba za mawasiliano ya simu *(National Numbering Plan)*. Ni kosa la kisheria kwa mtu binafsi au taasisi yoyote kutumia namba yoyote kinyume cha matumizi husika hususani kwa kutoa au kupokea taarifa kwa Umma.

Namba kwa ajili ya kuhabarisha umma kuhusu majanga hapa nchini hutolewa na TCRA kwa Mamlaka husika na sio vinginevyo. Yeyote atakayekiuka agizo hili atachukuliwa hatua za kisheria.

**Imetolewa na:**

**MKURUGENZI MKUU**
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**
**Mawasiliano Towers**
**20 Barabara ya Sam Nujoma**
**S.L.P. 474**
**14414 DAR ES SALAAM**
**TANZANIA**
**30 Aprili 2020**




Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya (katikati), akikagua uzalishaji wa ndoo katika kiwanda cha Silafrica Tanzania Ltd (Sumalia), ambazo zinatumika kunawia mikono ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: ELIUD RWECHUNGURA**.

# Mtambo uchenjuaji dhahabu kunusuru wakazi Nyamongo

**Na Ambrose Wantaigwa, TARIME**

MKOA wa Mara umeanza ujenzi wa mtambo wa kuchenjua madini katika eneo la uchimbaji dhahabu la Nyamongo ili kunusuru maisha ya wakazi na mifugo wanaozungukwa kutokana na kemikali za sumu wakati wa uchenjuaji.

Ofisa Madini mkoani Mara, Nyaisara Mgaya, alisema hatua hiyo imechukuliwa baada ya kubainika wachimbaji wadogo wanaozunguka mgodi wa dhahabu wa North Mara wameendelea kutumia kemikali zenye sumu ikiwamo zebaki kinyume cha taratibu za uhifadhi mazingira.

Alisema wiki iliyopita ng'ombe 34 na kondoo mmoja walikufa kutokana na kunywa maji yanayosadikiwa kuwa na sumu kutoka katika kituo kimojawapo cha kuchenjulia dhahabu cha binafsi katika Kijiji cha Kewanja ambapo idara ya mifugo wilayani Tarime iliamuru mizoga hiyo izikwe.

"Tayari hatua sahihi zimechukuliwa kukabiliana na tatizo hilo, ambapo mmiliki wake ameelekezwa kusitisha shughuli za uchenjuaji mara moja, na kurekebisha mfumo wa utoaji majitaka, huku akiamriwa pia kulipa fidia ya mifugo yote iliyokufa kutokana na uzembe," alisema Mgaya.

Alisema sambamba na ujenzi wa kituo hicho ofisi yake itaendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wachimbaji wote wadogo katika mji wa Nyamongo yatakayowajengea uwezo wa namna bora ya matumizi ya kemikali wakati wa uchenjuaji ili kuepuka madhara kwa wanadamu na mifugo.

Mgaya alifafanua kwamba sambamba na ujenzi wa mtambo wa kisasa wa kuchenjua madini, pia wataalamu wa madini wakishirikiana na Baraza la Taifa la Uhifadhi Mazingira (NEMC) wanaendelea na kuchukua sampuli za maji na udongo kwa ajili ya kubaini usalama wa vyanzo vya maji vinavyotumiwa na wananchi wa kawaida ukiwamo Mto Tigithe.

Mgaya alisema wachimbaji wadogo katika migodi yote isiyo rasmi mkoani hapa, wameelekezwa kusitisha shughuli zao kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha. Hali hiyo imesababisha wengi wao kukosa vifaa vya kisasa na kukosekana mifumo ya utoaji majitaka katika maeneo hayo.

"Kuna migodi mingi isiyo rasmi, ambayo haijapewa kibali na kulazimisha kufanya kazi za uchimbaji na uchenjuaji wa madini kinyume cha utaratibu...kuanzia sasa tumeagiza wasitishe uzalishaji wowote hadi hapo watakapotimiza masharti yanayosimamia sekta ya madini nchini," alisema. Mwenyekiti wa Kijiji cha Kewanja ambapo vilitokea vifo vya mifugo, Marwa Bunini, alisema baadhi ya wachimbaji wadogo wamekuwa wakikaidi maelekezo yanayotolewa na kamati ya mazingira ya kijiji yanayotaka kwanza kituo au mgodi upate kibali cha mazingira kutoka NEMC.

# Uboreshaji uhifadhi, utalii ikolojia Vikindu waanza rasmi

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umesema umeanza kuboresha shughuli za uhifadhi, utalii ikolojia pamoja na kukomesha uvamizi katika msitu wa Vikindu wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa TFS Kanda ya Mashariki ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, Caroline Malundo, wakati wa kukabidhi jengo la Ofisi za TFS lenye vyumba vya ofisi 14 lililogharimu zaidi ya Sh. milioni 437 lililojengwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

Alisema utalii wa ikolojia umeanzishwa katika msitu wa Vikindu, na kwamba ni vema Watanzania wakatumia fursa hiyo kwenda kufanya utalii wa ndani kwa kujifunza mambo yaliyopo katika msitu huo.

"Tumelenga kuimarisha utalii wa ikolojia, hii ni fursa kwa Watanzania kutembelea hifadhi hizi kwa sababu kuna vivutio vya kutosha na ndiyo maana TBA kupitia ofisi ya Meneja wa Mkoa wa Pwani ulipewa mkataba wa usanifu wa mradi wa kujenga ofisi bora za TFS katika wilaya hii ya Mkuranga ili kuwasaidia watumishi wafanye kazi kwa ufanisi na kuingiza pato la taifa," alisema Malundo.

Malundo alisema kukamilika kwa jengo hilo pia ni kutekeleza mpango mkakati wa pili wa TFS wa kuboresha maeneo katika hifadhi zake zote.

"Tuliona tuwe na jengo ndani ya msitu huu wa Vikindu ili kuboresha na kuimarisha hifadhi ya msitu huu, baada ya kuwapo kwa changamoto ya uvamizi uliokuwa unafanyika na kusababisha kuzorotesha nguvu kubwa ya uhifadhi katika eneo hili," alisema Malundo.

Aliongeza: "Hivyo uamuzi wa kujenga jengo hili ulikuja baada ya kuona kuna haja ya kuboresha hifadhi yetu hii ya Vikindu, tunaamini kwa sasa uvamizi wote uliokuwa unafanyika kwenye msitu huu hautakuwapo tena."

Mbunifu majengo wa TBA Mkoa wa Pwani, Greyson Kanyaburugo, alisema jengo hilo limekamilika na liko tayari kwa matumizi.

# 'NFRA lazima iwe kibiashara'

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imeweka bayana mpango mkakati wa kuhakikisha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) unajiendesha kibiashara na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alibainisha mkakati huo jijini Dodoma mwishoni mwa wiki, alipofunga kikao kazi cha Bodi ya Ushauri ya NFRA.

Mgumba alisema serikali imetathmini mwenendo wa NFRA katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo na kujiridhisha kuwa umeanza kutekeleza majukumu yake ipasavyo, hivyo kuongezewa jukumu muhimu la kununua nafaka kwa ajili ya kuhifadhi chakula na kujiendesha kibiashara.

Aliutaka wakala huo kufanya ununuzi wa mazao kwa ajili ya kuhifadhi kama akiba kwenye maghala ya serikali, lakini kwa ajili ya biashara kwa kutafuta masoko ndani na nje ya nchi.

Naibu Waziri Mgumba alisema wakala huo una jukumu la kuhifadhi mazao ya kila aina na siyo kuchagua mazao ya kuhifadhi, akitolea mfano mahindi kuwa ndiyo yamekuwa yakipewa kipaumbele kulinganisha na mazao mengine.

Alisema serikali imetekeleza maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa, hivyo NFRA inapaswa kuhakikisha inanunua nafaka ya kutosha kwa ajili ya kuhifadhi na kufanya biashara.

Mgumba alisema NFRA inapaswa kununua mahindi, mpunga na mtama kwa kuwa mazao hayo ni fursa kutokana na uhitaji mkubwa wa chakula nchini na nje ya nchi.

"Unaweza kuwa na fedha nyingi, lakini kama huna mipango mizuri ya ununuzi, huwezi kupata mazao. Hivyo, NFRA ni lazima mjipange vizuri ikiwamo kuongeza vituo vya ununuzi.

"Msije mkanunua mahindi kisiasa, ni lazima mtenganishe siasa na biashara. Mkifanya hivyo, mtajichimbia shimo wenyewe, hivyo lazima mkafanye biashara kwa ajili ya kupata faida," aliagiza.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Yustas Kongolle, aliishukuru Wizara ya Kilimo kwa kuwaamini yeye na wajumbe wa bodi hiyo kiasi cha kuwateua kuhudumu kwa miaka mitatu huku akisema watafanya kazi kwa bidii na weledi mkubwa zaidi.

"Kuaminiwa na wizara maana yake nchi imetuamini, tunaahidi kufanya kazi kwa bidii na kutimiza maagizo yote ambayo tumeelekezwa kufanya ikiwa ni pamoja na kuifanya NFRA ijiendeshe kibiashara," aliahidi.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Delphina Mamiro, ambaye ni Mjumbe wa Bodi hiyo ya NFRA, alisema bodi hiyo imejipanga kufanya kazi kubwa na nzuri zaidi.

Alisema mradi wa ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa utakamilika hivi karibuni, hivyo kuna jukumu kubwa na muhimu la kuhakikisha utekelezaji wa ununuzi unakamilika kwa wakati.

# Kortini madai ya rushwa ya 200,000/-

**Na Hamisi Nasiri,** NACHINGWEA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ( Takukuru) mkoani Lindi, imewafikisha watu wawili mahakamani akiwamo kaimu Ofisa Mtendaji Kata ya Kipara Mtua wilayani Nachingwea, Allen Mpira kwa kosa la kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. 200,000.

Mtuhumiwa mwingine ambaye amefikishwa mahakamani ni mkulima, Yahya Membe, mkazi wa Nachingwea.

Washtakiwa hao wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi.

Akisoma mashtaka ya washtakiwa hao, Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Osbon Mulamuzi, alidai kuwa washtakiwa hao wakiwa katika Kijiji cha Kipara Mtua walishawishi na kumuomba rushwa ya Sh. 200,000 kutoka kwa wanawake wawili, wakazi wa kijiji hicho.

Mulanuzi alidai wanawake hao waliombwa rushwa hiyo baada ya kutuhumiwa kuiba kuku, mali ya Yahya Membe.

Mulamuzi aliieleza mahakama kuwa kabla ya wanawake hao kuombwa kiasi hicho cha rushwa, walifikishwa katika ofisi ya Kaimu Mtendaji Kata ya Kipara Mtua, ambapo washtakiwa hao walipokea rushwa hiyo na dhamira yao ilikuwa kugawana fedha hizo.


Mwendesha mashtaka huyo aliendelea kudai kuwa washtakiwa hao waliwaomba rushwa wanawake hao ili wasiwachukulie hatua za kisheria kwa kosa lao la kuiba kuku.

Mulamuzi alidai maofisa wa Takukuru walipata taarifa na kuanza kuzifuatilia na kujiridhisha kuwa kilichokuwa kikiombwa na watuhumiwa hao wawili ilikuwa ni rushwa, jambo ambalo ni kosa la kushawishi na kupokea rushwa.

Mulamizi alidai kuwa watuhumiwa hao walikamatwa Oktoba 14, 2019 wakiwa wanapokea rushwa hiyo katika kijiji cha Kipara Mtua.

"Membe alikamatwa Oktoba 14, 2019 akiwa ofisini kwake na alikutwa akiwa na Sh.100,000, ambazo alipewa na wanawake hao," alidai Mulamuzi.

Mwendesha mashtaka huyo wa Takukuru alidai zaidi kuwa watuhumiwa hao wawili wamefunguliwa shtaka la kuwashawishi na kupokea rushwa, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria namba 11 ya mwaka 2007.




Mwambapa (kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janabi, mfano wa hundi ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya upasuaji wa moyo kwa watoto wanaotibiwa katika taasisi hiyo, ikiwa ni kukamilisha ahadi yake ya kuchangia kiasi cha Sh. milioni 100 ili kufanikisha upasuaji wa moyo kwa watoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CAG afichua upigaji mabilioni ya Pride

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini ubadhirifu wa mabilioni ya shilingi na mali za Kampuni ya Ukuzaji wa Juhudi za Maendeleo Vijijini (PRIDE).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, anafafanua kuwa, Pride ni kampuni iliyoanzishwa Mei 5, 1993 kuhamasisha maendeleo vijijini kupitia mradi wa maendeleo vijijini.

Anasema mradi huo unaendeshwa kwa ubia kati ya Serikali ya Kifalme ya Norway na Serikali ya Tanzania; na kwamba kuanzia mwaka 2015, ulitokea mgogoro juu ya umiliki wa Kampuni ya Pride kati ya Serikali ya Tanzania na wakurugenzi wa kampuni.

CAG anasema mgogoro ulihitimishwa kwa maagizo ya mahakama na makubaliano ya wakurugenzi wa kampuni kukubali kuwa kampuni ya Pride ni mali ya serikali.

"Kufuatia makubaliano haya, Januari 4, 2019, Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), iliiomba ofisi yangu kufanya ukaguzi wa kuhakiki mali na madeni ya kampuni hadi kufikia Oktoba 31, 2019 na kutathmini iwapo kulikuwa na ubadhirifu uliosababishwa na uwapo wa mifumo duni ya usimamizi katika uendeshaji wa kampuni kwa kipindi cha kuanzia Januari Mosi, 2017 hadi Desemba 31, 2019.

"Ukaguzi wangu ulibaini idadi ya mali na madeni ya kampuni hadi kufikia tarehe 31 Oktoba 2019, na uligundua uwapo wa ubadhirifu wa mali na madeni ya kampuni," anabainisha.

CAG anafafanua kuwa kampuni ina jumla ya mali zenye thamani ya Sh. bilioni 19.97 hadi kufikia Oktoba 31, 2019 zinazojumuisha mikopo ya wateja ya Sh. bilioni 8.82 na mikopo ya watumishi wake Sh. bilioni 11.14.

"Ukaguzi wangu juu ya uhalali na ukamilifu wa mali ulibaini kuwa mali zilizotajwa hazikuwa timilifu na kulikuwa na ubadhirifu kwenye mikopo iliyotolewa.

"Kampuni ya Pride ina utaratibu wa kutoa mikopo kwa watumishi wake ikiwa ni sehemu ya motisha ya utumishi. Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba 2019, kampuni ilikuwa inawadai watumishi wake kiasi cha Sh. bilioni 11.14. Mikopo hii ilikuwa kwenye makundi matatu, ambayo ni mkopo wa nyumba, mkopo maalum, na mkopo wa jumla.

"Ukaguzi wangu wa mifumo ya usimamizi wa mikopo (DUX) na usimamizi wa fedha (Bankers Realm) ulibaini kuwa, kiasi cha mikopo ya Sh. milioni 745.59 kinatokana na mikopo ya watumishi 168 walioacha au kuachishwa kazi, ambapo kampuni haina mkakati wowote wa namna ya kurudishwa kwake.

"Mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 10.38 ilitolewa kwa watumishi 33 bila makato ya urejeshaji kufanyika kwenye mishahara yao. Vilevile, ukaguzi uligundua mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 2.6 ambayo haikuwa na taarifa za wakopaji na hivyo kushindwa kujumuishwa kama sehemu ya mali za kampuni," anabainisha.

CAG anasema upungufu huo ulitokana na uwapo wa mifumo duni ya usimamizi katika kampuni na vitendo vya kibadhirifu vya watumishi waovu.

Ukiachia mikopo ya watumishi na wateja, CAG anasema ripoti ya mwisho ya mkaguzi wa nje ya mwaka wa fedha unaoishia Desemba 31, 2016, inaonyesha kampuni inamiliki mali zingine zinazojumuisha mali zisizohamishika, mali zinazohamishika za kudumu, hisa za kampuni, dhamana za muda mfupi na mrefu, pamoja na mali za kudumu zisizoshikika.

Hata hivyo, CAG anasema mali hizo hazikujumuishwa kwenye orodha ya mali za kampuni hadi kufikia Oktoba 31, 2019 kwa sababu mbalimbali kama vile hisa za uwekezaji zenye thamani ya Sh. bilioni 2.31 katika Benki M (Tanzania) zilizopotea baada ya benki hiyo kufilisika; dhamana za muda mrefu za Sh. bilioni 48.2 katika Benki za CRDB, Benki M (Tanzania) Limited, na NMB zilizotumika kulipia madai ya mikopo katika benki hizo.

Zingine ni mali zisizohamishika (Sh. milioni 942.11); na mali za kudumu zisizoshikika (Sh. milioni 956.46). CAG anasema mali hizo zote hazikuripotiwa kwa kuwa rejista ya mali haikuainisha gharama za mali moja moja, badala yake ikawekwa tarakimu moja ambayo ukaguzi wake ulishindwa kuthibitisha uhalali na usahihi wake.

"Kipande cha ardhi chenye viwanja namba 1 & 2 vyenye hati Na. 392106 katika Kitalu A mkoani Morogoro chenye thamani ya Sh. bilioni 1.44 hakikuripotiwa kwa kuwa thamani yake ya wakati wa ukaguzi (Januari 2020) haikujulikana.

"Ninapendekeza kuwa hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa watumishi waliohusika katika ubadhirifu wa mikopo ya wafanyakazi. Pia, mthamini wa mali wa serikali afanye tathmini kujua thamani ya mali ambazo hazikujumuishwa kama mali za kampuni kwenye ripoti hii," anashauri.

CAG pia anasema, ukaguzi wake ulibaini kampuni ilikuwa na madeni ya jumla ya Sh. bilioni 130.11 hadi kufikia Oktoba 31, 2019 na kwamba, wakati wa kutathmini ukamilifu na uhalali wa madeni yaliyotambuliwa, aligundua madeni matano kati ya saba ya madeni toka taasisi za fedha za nje ya nchi kutoka Stromme Foundation, Incofin, Responsibility, NMI Fund III KS, na Symbiotics yenye jumla ya Sh. bilioni 47.68, hayakuwa yamesajiliwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

"Hivyo, ukaguzi wangu ulishindwa kuthibitisha usahihi wa thamani ya madeni haya. Madeni ya Sh. milioni 361.76 toka kwa watoa huduma, hayakuthibitishwa kwa kukosa viambatisho vya hati ya madai na mikataba.

"Hakukuwa na taarifa za mwendelezo baada ya Desemba 31, 2018 wa makato ya wafanyakazi wa Pride yaliyokuwa yanakatwa na kampuni kwa ajili ya kikundi cha Saccos cha (Fahari Yetu Saccoss) ya kiasi cha Sh. bilioni 4.95 kwa sababu mfumo wa taarifa wa Saccos hiyo uliharibika na hapakuwa na taarifa mbadala.

# JKU yashauri wakazi Pemba kufuga samaki

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KIASI cha kilo 209 za samaki aina ya mwatiko wenye thamani ya zaidi ya Sh. milion 1, zimevuliwa na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) katika kituo cha Muambe Mkoa wa Kusini Pemba, huku wakazi wa maeneo jirani wakishauriwa kujikita katika ufugaji wa kitoweo hicho.

Akizungumza baada ya uvuaji wa samaki hao, Mkuu wa kituo cha JKU Muambe, Kaptein Issa Bakar Othman, alieleza samaki waliovuliwa wamechukua miezi tisa tangu kuingizwa katika mabwawa yao wakiwa vifaranga.

Akizungumzia ushirikiano na wakazi walio pembezoni mwa kambi hiyo, Kaptein Issa alisema wanashirikiana vizuri katika shughuli mbalimbali za kijamii.

"Hapo awali tulipoanza kufanya mradi huu kulikuwa na tatizo la baadhi ya vijana wa maeneo ya karibu na kambi yetu kuvamia mabwawa yetu na kuharibu miundombinu pamoja na kuwavua samaki waliomo kwenye mabwawa, lakini baada ya kukaa na wazee wa kijiji na kuzungumza nao, tabia hiyo imeachwa," alisema Kaptein Issa.

Akitoa wito kwa jamii hasa wale ambao wanaishi karibu na bahari kuanzisha mradi wa ufugaji samaki, kwani una faida kubwa.

"Mradi huu una faida kubwa sana kwani ukizingatia kuwa hivi sasa kilo moja ya samaki ni kati ya shilingi 7,000 hadi 8,000," alisema.

Naye mtaalamu wa ufugaji samaki JKU Muambe, Sajent Bakari Hamad, alieleza kuwa changamoto kubwa ambazo wanakabiliana nazo katika mradi huo ni mabadiliko ya hali ya hewa ambapo muda mwingine maji ya bahari hayaingii inavyotakiwa.

Aidha, kufa kwa vifaranga au kuliwa na baadhi samaki ambao huwa wanapenya kutoka baharini na kuingia katika mabwawa yao.

# Sekondari kujifunza kwa mtandao

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza imeandaa programu ya kuwezesha wanafunzi wa shule za sekondari kujifunza kwa njia ya mtandao katika kipindi hiki wakiwa nyumbani kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona (COVID-19).

Pia imewasisitiza wazazi kuwawezesha wanafunzi hao kupata maswali kupitia simu zao za viganjaji, vituo vya redio, runinga na kufuata vitini vya maswali katika shule wanazosoma watoto wao.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Shukrani Kyando, wakati akiwasilisha taarifa kwenye Baraza la Madiwani, na kuwasisitiza wazazi kuwasimamia wanafunzi kufuatilia vipindi vinavyotolewa kwa njia ya redio na runinga.

Pia alitoa wito kwa viongozi wa mitaa na kata wawasisitize wazazi kusimamia watoto wao kubaki majumbani katika kipindi hiki cha ugonjwa.

Diwani wa Kawekamo, Japhes Rwehumbiza, alihoji wanafunzi wa msingi watakuwa upande gani katika kipindi hiki, na kuomba nao wafanyiwe utaratibu wa kuendelea na masomo kwa njia ya mtandao, huku akiiomba halmashauri kuwasaidia walimu wa shule za binafsi kwani wanasaidia serikali katika kufundisha watoto.

Naye Diwani wa Viti Maalumu (CCM) Kata ya Buswelu, Rosemary Mwakisalu, alisema suala la utoaji elimu kwa njia ya mtandao siyo wazazi wote wana simu janja za kuwawezesha kupata maswali hayo.

Pia alisema wengine hawana redio wala runinga, na baadhi ya wanafunzi wanaishi vijijini wanaishi na bibi au babu, ambao ni wazee, hivyo hawajui namna walimu wanavyofundisha.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba idara ya elimu kupitia kwa mkurugenzi wajaribu kuangalia namna gani wanaweza kuboresha zaidi na kuhakikisha hadi watoto walioko vijijini wanapata huduma hiyo ya masomo.



Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania PLC, Hisham Hendi, akipimwa joto na askari wa duka la Vodacom, Masafa Hamad Muba jijini Dar es Salaam. Lengo la hatua hiyo ni kuwalinda wateja wake katika kipindi hiki cha ugonjwa wa corona, kwa kusisitiza uvaaji wa barakoa, kuwapima joto na kuwapa vitakasa mikono wateja waingiapo katika maduka yake kupata huduma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Bil. 3.2/- zakopesha wanawake Ilala

**Na Beatrice Philemon**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam, imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 3,223,070,000 kwa vikundi 517 vya wanawake wajasiriamali ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Ofisa Habari wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Tabu Shaibu, alisema fedha hizo zilitolewa kuanzia mwaka 2014 hadi Machi mwaka huu.

"Wanawake waliokopeshwa fedha hizo ni waliojikita katika biashara ya uzalishaji bidhaa za usafi, usindikaji, uzalishaji wa bidhaa za urembo na mapambo, usafirishaji, utoaji wa huduma za chakula na mapambo, ufugaji ukiwamo ukulima wa kisasa," alisema.

Alisema fedha hizo zilitolewa kulingana na mahitaji yao kupitia mfuko wa kuendeleza wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri husika.

Kadhalika, alisema Halmashauri ya Ilala imeendelea kuwezesha wanawake kiuchumi kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia sera na mwongozo wa uwezeshaji wanawake kiuchumi.

Alisema manispaa imekuwa ikitumia fursa ya majukwaa ya wanawake katika ngazi zote kuanzia mtaa, kata, wilaya, mkoa na taifa) ili kuendelea kujielimisha na kupambanua mianya ya kujihusisha na fursa za ndani na nje ya nchi kiuchumi.

Pia vikundi vya kiuchumi kama SACCOs, VICOBA na vingine vinavyosajiliwa na kutambuliwa toka ngazi ya wilaya hadi Taifa.

Vilevile upatikanaji wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wanawake wadogo, wakubwa na wa kati na kutumia mifuko 20 ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. "Moja ya mifuko hii ni mfuko wa kuendeleza wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri husika," alisema.

Akielezea vikundi vya kiuchumi kama Saccos, Vicoba na vikundi vingine vilivyosajiliwa na kutambulika toka ngazi ya wilaya hadi Taifa, alisema uhamasishaji wanawake kuhusu usajili wa vikundi umefanyika kwa asilimia 311, ambapo mpaka mwaka 2019/2020, jumla ya vikundi 1935 vya wanawake vimesajiliwa na kutambuliwa kisheria kwa kupewa vyeti.

"Vyeti hivi ni utambulisho kuwa vikundi hivi vinatambulika na vinaweza kutumika sehemu nyingine yoyote kama utambulisho wa kufahamika ndani ya halmashauri.

Pia halmashauri imesimamia na kufuatilia uanzishwaji wa majukwaa ya wanawake katika ngazi ya kata, mtaa na kupata viongozi wa kuchaguliwa.

"Majukwaa haya ni muhimu sana katika kuwezesha wanawake kiuchumi kwa kutoa fursa ya wanawake kukutana na kubadilishana uzoefu wa shughuli za kiuchumi wanazofanya," alisema na kuongeza:

"Kupashana habari ya fursa mbalimbali zilizopo kama mitaji, masoko na kuwaunganisha na taasisi mbalimbali za uwezeshaji kama NEEC, SIDO, GSI, TFDA (sasa TMDA), TANTRADE, TRA, TAFOTA, GMT, na taasisi za kifedha."

Alisema uzinduzi wa jukwaa la wilaya umefanyika na kuwezesha uzinduzi katika ngazi ya kata, alisema hadi sasa kata 30 zimekwisha zindua majukwaa hayo na maandalizi ya uzinduzi wa makujwaa katika kata zilizobaki yanaendelea.

Shaibu alisema halmashauri imeweza kufanya maonyesho ya wajasiriamali kupitia viwanja vya halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, na jumla ya vikundi vya wanawake 688 vilishiriki maonyesho hayo.

Nipashe
Spotika




MASTRAIKA 6 WAKIGENI WANAOWINDWA YANGA UK. 14




# KWA NINI WILLIAN SI JIBU STRAIKA LIVER

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo amefikisha mabao 40 katika kila msimu kwa misimu tisa, na kwa sasa ana jumla ya mabao 743 kwa jina lake, na akifunga mabao matatu zaidi atavunja rekodi ya gwiji Ferenc Puskas, huku akifunga mabao 24 zaidi atakuwa na mabao mengi zaidi kuliko Pele.

**LIVERPOOL,** England

KWA uhakika kabisa Liverpool ina kikosi bora zaidi cha kwanza. Kila mchambuzi amekuwa akiimba kwa namna gani kikosi hicho cha kocha Jurgen Klopp kilivyoimarika.

Hata hivyo, kumekuwa na kelele kwamba, kocha huyo raia wa Ujerumani anahitaji kukiongezea nguvu kikosi chake. Huku wachezaji wengi wakipanga kuondoka katika dimba la Anfield kipindi cha majira ya joto, hitaji hilo linazidi kukua. Dejan Lovren, Adam Lallana na Xherdan Shaqiri; ambao wote wamekuwa wakikaa zaidi bechi pale Anfield watakuwa wanaondoka kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

Na wachambuzi wanaona kwamba, kuondoka kwa wachezaji hao watatu kunatakiwa kufanyiwa kazi haraka. Klopp ameripotiwa anawania kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Willian, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 akiwa anatarajiwa kuondoka pale Stamford Bridge baada ya kushindwa kukubaliana kwenye maslahi yake binafsi ili asaini mkataba mpya.

Hivyo, Willian anaonekana kuelekea kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ulaya (labda) na Liverpool watampata raia huyo wa Brazil akiwa mchezaji huru, nini kitakwenda mrama?

Makala haya yanakuelezea sababu mbili kwa nini Willian hataweza kufiti kwenye mfumo wa Liverpool.

### UMRI

Katika umri wake wa miaka 31, winga huyo wa Chelsea hatakuwa tayari kuona siku zake za mwisho za uchezaji zikimalizikia benchi pale Anfield, atakuwa anataka kucheza mara kwa mara. Nafasi hiyo ipo kwa Mohamed Salah na Sadio Mane.

Hakuna shaka juu ya ubora wa Willian kwenye kumiliki na kugawa pasi. Tangu awasili pale Chelsea mwaka 2013, ametwaa mataji mawili ya Ligi Kuu, moja la FA, la Ligi na Ligi ya Europa, bila kujali mechi 70 alizoichezea Brazil. Lakini sasa umri wake unaonekana kumtupa mkono na hata kasi yake dimbani imepungua kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo, mazungumzo kati yake na Chelsea inaelezwa yamevunjika kutokana na yeye kusisitiza anataka mkataba wa miaka mitatu. Klabu hiyo ya Stamford Bridge haikuwa tayari kutoa ofa hiyo, kwani maana yake mkataba wake ungekuwa ukimalizika wakati akikaribia miaka 35.

Katika kikosi kinachocheza mara kwa mara cha Klopp, ni wachezaji wanne tu ndio wenye umri zaidi ya miaka 30 ,wawili kati yao ni (Lovren na Lallana) ambao wataondoka kipindi cha majira ya joto na watatu ni golikipa, Andy Lonergan. Kikosi cha Klopp kimejengwa na wachezaji wenye umri wa katikati ya miaka 20 na si 35.

### MFUMO

Staili ya uchezaji ya raia huyo wa Brazil, ndio moja ya sababu ambayo Chelsea imekuwa ikipoteza kwa haraka mipira ya mbele na kurudi nyuma. Mara nyingi Willian ni mchezaji hatari kwa mipira 'iliyokufa' na mwepesi kurudisha mpira nyuma.

Hiyo si staili ya uchezaji kwa kikosi cha Klopp, kwani mara zote mpira unasukumizwa mbele. Kwa sasa mchezaji muhimu zaidi katika mfumo wa Klopp katika nafasi ya kiungo mshambuliaji ni Roberto Firmino. Mara zote fowadi yake inahitaji kuwa na mpira huku msaidizi wao akiwa na uwezo wa kuumiliki.

Washambuliaji Mohamed Salah na Sadio Mane wanahitaji msaidizi mwenye uwezo wa kukaa na mpira na kuwalisha mara kwa mara na si kurudisha nyuma kuanza tena.

Na kazi hiyo kwa sasa inamfiti zaidi Firmino na hivyo, Liverpool ikicheza inaonekana kama ina washambuliaji watatu mbele, kwa sababu wao mara zote wanahitaji kusukumiziwa mpira mbele na kutafuta mabao.

Na mfumo huo umewafanya Mane na Salah kufunga mabao 46 na 70 kwenye Ligi Kuu kwa misimu mitatu iliyopita.

Mabao ya Liverpool yanatokana na pasi ndefu na hivyo ndio mfumo wa Klopp unavyofanya kazi. Katika misimu saba za Ligi Kuu ya England, Willian amefunga mabao 33 ya Ligi Kuu.

Liverpool kwa misimu miwili iliyopita kikosi chake cha kwanza ni kilekile maana yake ni kwamba mfumo wake unafanya kazi vizuri zaidi.

Hivyo hakuna sababu yoyote itakayoilazimu Liverpool kuwa na mahitaji ya huduma ya Willian kwenye kikosi chake, kwani haendani na mfumo wao wa uchezaji.

# MASTRAIKA 10 BORA DUNIANI KWA SASA


KYLIAN MBAPPE

**LONDON,** England

WAKATI ni sawa kuwasifia magolikipa, walinzi na viungo kwa mchango wao kwenye mafanikio ya timu, nguzo kuu ya ushindi kwenye mchezo inabaki kuwa rahisi: kufunga mabao mengi kuliko mpinzani wako.

**Maana yake ni kwamba kutafuta mafanikio ya uhakika kwenye daraja la juu, unahitaji mshambuliaji wa ukweli. Kwa sasa kuna idadi kubwa ya washambuliaji wa juu katika mchezo wa soka duniani, kwa mastraika hao kufunga mabao katika ligi mbalimbali duniani kutoka England na Hispania hadi Italia na Ujerumani.**

Na hilo linafanya kuwa jambo gumu kuwataja washambuliaji bora duniani, kwa sababu wapo wengi wa kiwango cha juu na cha kuvutia kabisa.

Ni heshima kuwataja; Jamie Vardy wa Leicester City kwa sasa yupo katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora wa Ligi Kuu ya England msimu wa 2019-20. Huku pia Luis Suarez wa Barcelona kwa miaka mingi ametambulika kama mmoja wa mshambuliaji bora kabisa. Raia huyu wa Uruguay alionyesha cheche zake pale Liverpool hadi sasa kule Nou Camp. Na Neymar wa Paris Saint-Germain, hakuna swali kuhusu kipaji chake. Raia huyu wa Brazil ni mchezaji mwenye uwezo wa kila aina katika kufunga mabao na msimu huu ana mabao 18 kutoka mguu mwake kwenye mechi 22. Makala haya yanakuchambuliaji washambuliaji10 bora wa soka duniani, twende sasa...

### #1. SERGIO AGUERO (MANCHESTER CITY)

Licha ya kwamba ameingia kwenye umri wa miaka 32, mshambuliaji huyu wa Manchester City, Sergio Aguero haonyeshi ishara ya kushuka kiwango linapokuja suala la kufunga. Ameongeza mabao 23 katika mechi 30 msimu wa 2019-20. Na kuna nafasi kubwa kwake msimu huu ukirudi kuweza kushinda Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi Kuu ya England.

Ni mmaliziaji mzuri na hana masihara akiwa ndani ya boksi, kwani anaweza kukufunga kwa mguu au kwa kichwa.

Tangu alipojiunga na Man City mwaka 2011, alikosa msimu mmoja tu kufikisha mabao 20 na amevuka idadi ya mabao 30 katika misimu mitano. Kwa sasa raia huyu wa Argentina yupo nafasi ya nne kwenye orodha ya wafungaji wanaoongoza kwenye Ligi Kuu ya England.

### #2. ROBERT LEWANDOWSKI (BAYERN MUNICH)

Mshambuliaji wa kimataifa wa Poland, Robert Lewandowski kwa muda mrefu amekuwa akitajwa kama mmoja wa washambuliaji bora kabisa katika sayari hii, lakini msimu huu, amepaa zaidi. Akiwa na umri wa miaka 31, amefunga mabao 25 kwenye mechi 23 za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akiwa na Bayern Munich. Na kule kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ndiko kabisa amefunga mabao 11 katika mechi sita tu.

Amekuwa na kiwango cha juu zaidi msimu huu akiwa na klabu yake, kwani pale aliposhindwa kufunga alitoa pasi ya mwisho na zimefika tano kwa Bayern hadi sasa. Msimu wa 2019-20 pengine ndio bora zaidi kwake hadi sasa, lakini kwa ufungaji mabao nchini Ujerumani tayari amekuwa gwiji. Katika misimu yake sita kwenye Bundesliga, amefunga mabao 202 katika mechi 290.

### #3. HARRY KANE (TOTTENHAM HOTSPUR)

Nahodha wa sasa wa England, Harry Kane, amekuwa na wakati mgumu msimu huu kutokana na kusuasua kwa timu yake na yeye kuumia misuli ambapo amekuwa nje ya dimba tangu mwanzoni mwa mwaka huu. Hata hivyo, amekuwa na uwezo wa kufunga mabao 11 kwenye Ligi Kuu na sita kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mechi tano alizocheza.

Kane alipewa nafasi ya kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Spurs msimu wa 2014-15, na tangu hapo hajaangalia nyuma. Msimu huo alifunga mabao 31, na aliendelea na rekodi hiyo kwa kufunga mabao 181 katika mechi 278 zote alizoichezea klabu hiyo.

Katika ngazi ya kimataifa amekuwa na mafanikio makubwa; alishinda Kiatu cha Dhahabu kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018 akiwa na England. Hivi karibuni alifunga mabao 12 wakati wa kufuzu kwa Euro 2020, mengi kuliko mchezaji yeyote.

### #4. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS)

Pengine ni mchezaji bora wa wakati wote, ni ngumu mno kuyaelezea mafanikio yote ya Cristiano Ronaldo. Kwa nyakati alizocheza Manchester United, Real Madrid na Juventus, raia huyu wa Ureno ameshinda mataji sita ya Ligi Kuu na matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, pamoja na moja la Mataifa ya Ulaya na Ligi ya Mataifa ya Uefa kwenye ngazi ya kimataifa.

Ronaldo alianza kucheza soka kama winga, lakini taratibu akabadilika na kuwa straika. Amefikisha mabao 40 katika kila msimu kwa misimu tisa, na kwa sasa ana jumla ya mabao 743 kwa jina lake.

Akifunga mabao matatu zaidi yatamfanya kuivunja rekodi ya gwiji Ferenc Puskas, huku akifunga mabao 24 zaidi atakuwa na mabao mengi zaidi katika maisha yake ya soka kuliko Pele.

### #5. LIONEL MESSI (BARCELONA)

Ni mchezaji pekee ambaye bado anacheza kwa sasa ambaye ana rekodi ya kulinganishwa na Cristiano Ronaldo, ni nyota wa Barcelona, Lionel Messi ana hatua mbili tu zimebakia kuwa kwenye orodha ya mfungaji bora wa wakati wote. Amefunga jumla ya mabao 724 kwa jina lake hadi sasa, ikiwa amepitwa 19 na Ronaldo, lakini amecheza mechi pungufu 100 kuliko mpinzani wake.

Kama ilivyo kwa Ronaldo, ni rahisi kusema kwamba, raia huyo wa Argentina ni mchezaji bora wa wakati wote.

Messi anashikilia rekodi ya ufungaji mabao kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga. Amefunga mabao mengi zaidi katika historia ya ligi hiyo (438). Amefunga 'hat-trick' nyingi zaidi kwenye historia ya LaLiga (36) na pia ndiye mwenye pasi za mwisho nyingi zaidi (181).

Juni mwaka huu atafikisha umri wa miaka 33; ingawa anaelekea mwisho wake wa uchezaji, bado amefunga mabao 24 msimu huu.

Amebeba tuzo ya Kiatu cha Dhahabu Ulaya mara sita (mfungaji bora wa ligi kubwa tano Ulaya) ni ngumu kwa mchezaji mwingine kwa sasa kufikia rekodi hiyo.

### #6. CIRO IMMOBILE (LAZIO)

Mashabiki wengi kwa urahisi tu wanaweza kuhoji kuwa mshambuliaji huyu wa Lazio, Ciro Immobile, hasitahili kuwapo kwenye orodha hii. Raia huyo wa Italia ana umri wa miaka 30, sasa na wakati anahamia kwenye uwanja huo wa Olimpico mwaka 2016, hakuwa na kiwango cha kufunga mara kwa mara. Lakini kwa sasa, pengine hakuna mshambuliaji mwenye kiwango bora kwa ufungaji kama yeye barani Ulaya.

Kwa sasa anaongoza katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya kwa msimu 2019-20. Amefunga mabao 27 katika mechi 26 za Ligi Kuu kwa Lazio. Hayo ni sita zaidi ya Cristiano Ronaldo aliyofunga. Lakini Immobile si mgeni kwa ufungaji wa mabao kwenye Ligi ya Serie A amekuwa mfungaji bora mara mbili.

### #7. MOHAMED SALAH (LIVERPOOL)

Ni ngumu kumtaja nani straika bora wa Liverpool, lakini ni sawa kabisa kuwa Mohamed Salah amekuwa na mafanikio makubwa mno tangu alipotua kwenye klabu hiyo kipindi cha majira ya joto mwaka 2017.

Virgil van Dijk na Alisson Becker wameifanya safu ya nyuma kuwa imara, lakini ujio wa Salah umeifanya pia fowadi yao kuwa ya kutisha.

Akiwa ametua kutoka Anfield baada ya mafanikio mazuri pale Roma, Salah alifunga mabao 44 msimu wa 2017-18. Mabao 32 yalikuwa kwenye Ligi Kuu na kumpa Kiatu cha Dhahabu. Ikafuatiwa na kufunga mabao mengine 27 katika msimu wake uliofuata, na pia akachukua Kiatu cha Dhahabu.

Kwa sasa kwa jina lake ana pasi za mwisho 24 kwenye Ligi Kuu ya England tangu alipojiunga na Liverpool.

### #8. SADIO MANE (LIVERPOOL)

Liverpool ni moja ya timu zenye safu bora zaidi ya ushambuliaji duniani kwa sasa. Na huku tayari tumeshamjadili Mo Salah, 'Wekundu' hao wana mfungaji mwingine wa aina yake, Sadio Mane raia wa Senegal.

Msimu wa 2017-18, alifunga mabao 20, kati ya hayo 10 yalitoka kwenye Ligi Kuu. Lakini msimu wa 2018-19, ulimshuhudia akifunga mabao 26. Wakati ligi hiyo ikisimama Machi tayari alikuwa na mabao 14 katika mechi 26.

### #9. KYLIAN MBAPPE (PARIS SAINT-GERMAIN)

Pengine ndiye mchezaji kijana mwenye kipaji cha juu zaidi kwa sasa. Kylian Mbappe alichomoza kwenye msimu wa 2016-17 akiwa na Monaco, wakati alipowasumbua walinzi wa klabu kadhaa za Ulaya kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kikosi chake kikatinga nusu fainali.

Mshambuliaji huyo Mfaransa alifunga mabao 26, msimu huo akiwa na umri wa miaka 18 halafu akahamia kule Paris Saint-Germain, awali ikiwa kwa mkopo na baadaye kwa ada ya euro milioni 145. Tangu atue Paris, Mbappe amekuwa na kiwamgo bora zaidi. Alifunga mabao 31 katika msimu wake wa kwanza, halafu akaongeza hadi 39 katika mechi 43 msimu wa 2018-19. Msimu wa sasa amefunga mabao 30 katika mechi 33.

Katika ngazi ya kimataifa amekuwa moto, amefunga mabao 13 kwa Ufaransa yakiwamo manne kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018, ambapo aliisaidia nchi yake kutwaa ubingwa huo wa dunia na yeye kutwaa tuzo ya mchezaji bora kijana wa mashindano hayo.

Kama mshambuliaji gwiji wa Ufaransa, Thierry Henry, Mbappe ana uwezo wa kucheza nafasi ya mshambuliaji wa kati na pembeni huku akiwa na kasi kubwa. Na kwa sasa akiwa na umri wa miaka 21, ana nafasi ya kuja kuwa mshambuliajii bora duniani kwa siku zijazo.

### #10. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG (ARSENAL)

Usajili wa Januari mwaka 2018, ulishuhudia Arsenal ikivunja rekodi ya uhamisho kwa kulipa kiasi cha paui milioni 56 na kumtwaa mshambuliaji wa kimataifa wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang hadi kwenye dimba la Emirates akitokea Borussia Dortmund. Baada ya miaka miwili baadaye, imekuwa ni ngumu kwa mtu yeyote kuwalaumu kwa kutumia kiasi kikubwa cha fedha.

Tangu kuwasili kwenye Ligi Kuu ya England, Aubameyang bila shaka yoyote amethibitisha ubora wake kama mmoja wa washambuliaji bora kabisa duniani.

Baada ya kufunga mabao 98 katika mechi 144 za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akiwa pale Dortmund, amekuwa muaji zaidi kwenye EPL.

Kuanza kwake kwenye nusu ya msimu kulimshuhudia akifunga mabao 10 katika mechi 13, wakati msimu wa 2018-19 alitwaa Kiatu cha Dhahabu kwa kufunga mabao 22 katika mechi 36. Na kabla ya Ligi Kuu kusimama, tayari alikuwa na mabao 17 katika mechi 26.

Katika umri wake wa miaka 30, anaonekana bado ana mambo mengi ya kuionyesha dunia kwamba ana kipaji cha uchezaji soka na hasa kwenye kufunga mabao.

## Nukuu

"Hadi leo hii hakuna yeyote anayejua ukweli, sikuwa na maelewano na Mtendaji Mkuu, Ivan Gazdiz, na ndio maana niliamua kuondoka [Arsenal], suala la mimi kuweka masharti makubwa kwenye mkataba mpya halikuwapo na wao wakakataa kunipa mkataba mpya," **Robin Van Persie, akifichua siri ya kuachana na klabu hiyo na kutimkia Manchester United mwaka 2012.**



"Hatutabadilika, hicho ndio kitu cha kwanza, lakini kama tutakuwa bora itategemea na nini klabu nyingine zinafanya kwa sababu zote zina nafasi ya kuimarisha vitu, na kufanya vitu kwa ubora zaidi. Hivyo, sina shaka kuhusu majaliwa ya baadaye kwamba sisi tutaendelea kuwa bora. Lakini hatutabadilika. Timu hii haijamaliza kurasa, na tuna nafasi kubwa ya kuimarika na kufanya kazi vizuri," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp**




"Kila mmoja anapenda kuangalia fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na Tottenham walikuwa pale hivyo nilikuwa na hisia za hali ya juu, nilikuwa na matumaini wamefika fainali na watafanya kile walichokusudia. Kwa upande wetu mashabiki wa Tottenham ilikuwa fainali iliyotuumiza, lakini unatakiwa kuangalia picha kubwa. Walifanya kazi kubwa na kwa pale walipofikia," **Straika wa Real Madrid, Gareth Bale akielezea namna ambavyo bado anaihusudu Spurs.**






# MASTRAIKA 6 WAKIGENI WANAOWINDWA YANGA

MAKAMBO

**Na Adam Fungamwango**

NI kama vile Yanga imepania msimu ujao ije kivingine kutokana na jinsi inavyopambana kutaka kusuka kikosi chake ili kiwe na ushindani kuliko cha msimu huu.

**Viongozi wa Yanga wameshatambua kuwa kama Simba ya msimu uliopita na huu imekuwa maji marefu kwao, basi endapo hawajawekeza kwenye usajili wa maana, inawezekana kabisa kuwa msimu ujao ikala kwao.**

Hata msimu uliopita Yanga ilipocheza michuano ya Ligi ya Mabingwa, ilicheza kwa sababu kulikuwa na nafasi nne, laiti kama nafasi zingekuwa mbili, ingeyasikia michuano hiyo kwenye bomba.

Ina maana kwa misimu miwili, haitatizwi na Simba tu, bali hata na Azam FC ambayo nayo imekuwa na kikosi imara.

Pamoja na kuboresha maeneo tofauti, lakini inaonekana viongozi wa Yanga wamemulika zaidi idara ya ushambuliaji ambayo msimu huu imeonekana kuwa na matatizo.

Mwanzo wa msimu iliwashusha mastraika wa nje, Juma Balinya kutoka Uganda na Mnamibia Sadney Urkhob, lakini walionyeshwa mlango wa kutokea kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Kwa sasa upande wa straika tegemeo kubwa ni David Molinga ambaye ni Mkongomani, lakini kuna Muivoriani Yikpe Gnamien, straika ambaye uwezo wake haujawavutia wanachama na mashabiki wa Yanga mpaka sasa.

Ndiyo maana duru za michezo zimekuwa zikiwahusisha baadhi ya wachezaji wanaocheza nafasi ya straika na hata namba zingine ambao si Watanzania kuchukua nafasi kwenye klabu hiyo kongwe kwa msimu ujao. Hawa ni baadhi yao...

**HERITIER MAKAMBO-HOROYA AC**

Yanga inataka kumrudisha tena straika wake wa zamani, Heritier Makambo. Habari zinasema kuwa huenda straika huyo aliyeuzwa msimu huu kuelekea Horona AC ya Guinea akarejeshwa kwa ajili ya kuimarisha idara ya ushambuliaji.

Kura zote zimemwangukia kwa sababu ni mchezaji anayeijua vizuri Yanga na msimu uliopita alifanya vema, akifunga mabao 17, akiwa wa tatu nyuma ya Salim Aiyee wa Mwadui aliyemaliza na magoli 18 na Meddie Kagere wa Simba aliyetwaa Kiatu cha Dhahabu na mabao yake 23.

Makambo ndiye chaguo namba moja la Wanayanga wote na kuonekana kuwa ni mwarobaini wa uhaba wao wa mabao.

**MICHAEL SARPONG-RAYON SPORT**

Ni straika raia wa Ghana ambaye rada za Yanga zimeelekezwa kwake kwa ajili ya kumsainisha mkataba tayari kwa msimu ujao wa ligi.

Michael Sarpong anayeichezea Rayon Sport ya Rwanda, anatajwa kuwa huenda akasajiliwa na mabingwa hao wa kihistoria kutibu tatizo la upachikaji mabao kwenye klabu hiyo.

Inawezekana kabisa Yanga inapata urahisi zaidi kumsajili, kwani habari kutoka Rwanda zinasema kuwa straika huyo ametimuliwa na klabu hiyo kutokana na utovu wa nidhamu.

**MOZIZI MPIANA-FC LUPOPO**

Straika huyu Mkongomani naye anatajwa kuwa huenda akawa mmoja wa wachezaji watakaovaa jezi ya Yanga msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mpiana, anayeichezea Saint Eloi Lupopo ya nchini Congo, naye duru zinamtaja kuwa huenda akatua Jangwani na kumfuata Molinga kwa ajili ya kuboresha nafasi ya ushambuliaji kwenye kikosi hicho ambacho msimu huu kimeonekana ni butu.

**TUISILA KISINDA- AS VITA**

Kuna wakati hucheza kama winga na mara nyingine hucheza kama straika namba mbili, au msaidizi wa straika kwenye kikosi cha AS Vita ya DR Congo.

Naye anatajwa kuwaniwa na Yanga kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara. Hata hivyo, ni mmoja wa wachezaji ghali kabisa Afrika, hivyo kama wanamhitaji wavunje benki, si mchezo mchezo.

**ALLY NIYONZIMA- RAYON SPORT**

Ni mmoja kati ya viungo bora nchini Rwanda akiichezea Rayon Sport, lakini kwa siku za karibuni amekuwa akichezeshwa hata nafasi ya straika. Naye amekuwa akihusishwa kujiunga na klabu ya Yanga kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu.


Hata hivyo, duru zingine zinasema kuwa klabu kadhaa Ulaya, nazo zimekuwa zikimwania Niyonzima na klabu yake inaona kama huko itapata donge nono zaidi. Hata hivyo, lolote linaweza kutokea.

**BIGIRIMANA BLAISE- NAMUNGO**

Mrundi huyu anacheza soka la kulipwa hapa hapa nchini kwenye klabu ya Namumgo FC ya mjini Lindi. Imeelezwa kuwa amekuwa kwenye mazungumzo na klabu ya Yanga ili kutia saini kuitumikia kwa ajili ya msimu ujao wa ligi.

Blaise ambaye anacheza kama straika namba moja, lakini msaidizi wa straika namba moja, amekuwa kwenye kiwango kizuri msimu huu, akipachika mabao tisa mpaka sasa na kuifanya Namungo kuwa timu tishio msimu huu.

**JE, WAJUA?**



NI mshambuliaji wa Leicester City, Jamie Vardy pekee, aliyefunga mabao mengi (19) zaidi kwenye Ligi Kuu msimu wa 2019-20 kuliko Pierre-Emerick Aubameyang, ambaye alifunga mabao 22 msimu uliopita na kuwa mmoja wa wachezaji watatu waliotwaa Kiatu cha Dhahabu.





# Ashauri ulinzi zaidi mipakani tishio la corona

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MBUNGE wa Namtumbo (CCM), Edwin Ngonyani, ameiomba serikali kuongeza ulinzi zaidi katika maeneo ya mipakani ili kujikinga na ugonjwa wa corona.

Ombi hilo alilitoa jana jijini hapa alipokuwa akipokea msaada kutoka kwa taasisi isiyo ya kiserikali ya Furahika kwa ajili ya wananchi wake kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema ni muhimu kuimarishwa ulinzi ili wageni wasije ingia kupitia vichochoro na kuwaletea virusi vya corona.

Mbunge huyo alisema pamoja na wakazi wa eneo hilo kutambua uwapo wa ugonjwa huo, bado elimu zaidi inatakiwa kutolewa.

Alishukuru taasisi hiyo kwa kutoa Sh. 500,000 kwa ajili ya kununua barakoa na vitakasa mikono, huku akiomba taasisi nyingine zikumbuke kutoa misaada hasa kwenye wilaya zilizopo mipakani.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Furahika, Gaudence Msuya, alisema wameamua kutoa fedha kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za serikali kwenye mapambano hayo.

Alisema Namtumbo sio eneo la kwanza kupata msaada huo, bali walishatoa katika maeneo mbalimbali kusaidia kununua barakoa na vitakasa mikono.

Msuya alisisitiza wananchi kujikinga ili kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

"Tupo pamoja na serikali kuhakikisha tunasaidia kupambana na ugonjwa huo lengo ni kuona unaisha hapa nchini," alisema Msuya.

Alisema matarajio yao ni kuona kila mkoa unakuwa na barakoa pamoja na vitakasa mikono ambavyo ni kwa ajili ya watu kutumia kujikinga na ugonjwa wa corona.

Msuya alisema taasisi yao itaendelea na utaratibu huo, huku akiziomba na taasisi nyingine kuiga mfano huo ili kusaidia watu kujikinga.

"Unajua kazi ya kupambana na corona sio ya serikali pekee bali ni yetu sote, hivyo tujitahidi kusaidiana na serikali kuutokomeza ugonjwa huu, " alisema Msuya.

# Viongozi wa dini waombwa ushirikiano mapambano corona

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

VIONGOZI wa madhehebu ya dini wametakiwa kuungana na serikali katika kupambana na ugonjwa wa corona nchini.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, alipokuwa akizungumza kwenye semina elekezi kuhusu ugonjwa huo mashekhe, maimamu na walimu wa madrassa wa Wilaya ya Dodoma.

Mavunde alisema viongozi hao wanawajibu mkubwa wa kuungana kwa pamoja na serikali ili kuhakikisha ugonjwa huo unatokomezwa.

Alisema pamoja na jukumu walilonalo la kumuomba Mungu kwa ajili ya kuinusuru nchi, wao kama viongozi wa dini wana jukumu kubwa la kutoa elimu kwa waumini ili kujikinga na maambukizi ya corona.

"Nyinyi ndiyo mnaokutana na waumini wenu huko kwenye nyumba za ibada, hivyo kwa nafasi hiyo mnaweza kuisaidia serikali katika kuwaelimisha jinsi ya kujikinga na janga hili," alisema.

Kwa upande wake, Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, aliwataka viongozi hao kuchukua tahadhari kujiepusha na janga hilo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Dar-Ul-Muslimeen, Shekh Muslim Bhanji, aliwataka viongozi hao kutoa elimu kwenye familia zao.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Mavunde aliziomba taasisi, mashirika ya kidini kusaidia serikali vifaa mbalimbali vya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

Mavunde ambaye ni Mbunge wa Dodoma Mjini, alitoa kauli hiyo alipokuwa akikabidhi vifaa mbalimbali kwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ambavyo ni barakoa 200, majaba 20 ya lita 160 ya maji na madumu ya maji madogo 50 kwa ajili ya kusambaza kwenye maeneo yenye mikusanyiko ya watu.

Aliwataka wakazi wa Dodoma kutokuwa sehemu ya usambaza wa virusi vya corona, bali wachukue tahadhari ya kuepukana na janga hilo.

"Ninawaomba wananchi wa Dodoma tuzingatie maelekezo ya viongozi wetu wa serikali, wataalamu wa afya ikiwamo kuepukana na kukaa kwa kwenye mikusanyiko isiyo ya lazima," alisema.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Katambi, alisema vifaa hivyo vitasambazwa kwenye taasisi zinazohudumia mikusanyiko ya watu wengi.

Aliwataka wanasiasa kusaidia mapambano ya ugonjwa huo kwa kutoa elimu kwa jamii.

Mwenyekiti wa Chama cha Majaji na Mahakimu Tanzania kwa mkoa wa Dodoma, Cosmas Mataba, alisema misaada hiyo itasaidia kuondoa uhaba wa vifaa hivyo ambavyo katika ofisi zao ambazo zinahudumia watu wengi zaidi.

Alisema vifaa hivyo vitaokoa watumishi ambao wanawahudumia wananchi wanaofika kupatiwa huduma za kimahakama kila siku.



Baadhi ya wakazi wa Kisasa jijini Dodoma wakihakiki majina yao jana, kwenye kituo cha uandikishaji cha Njendengwa Mashariki kilichopo Shule ya Msingi Kisasa. Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetoa siku tatu kuanzia Mei 2 hadi leo kwa wananchi kuhakiki taarifa zao, na kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura kwa baadhi ya mikoa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Viongozi wapya wa CPC watakiwa kuwa waadilifu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

VIONGOZI waliochaguliwa wa Chama cha Waandishi wa Habari Dodoma (CPC), wametakiwa kuhakikisha wanawatumikia wanachama wao kwa uadilifu na kuwaletea fursa za maendeleo.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi wa chama hicho, Abubakari Famau, baada ya kutangaza matokeo ya uchaguzi wa viongozi hao ambao wataongoza kwa kipindi cha miaka mitano.

Alisema wanachama wanahitaji kuona CPC ikitoa fursa tele kwa wanachama wake ndani ya chama hicho, na kuwataka kuongeza idadi ya wanachama ili wote watambulike kupitia chama hicho.

Awali, akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Famau, alimtangaza Mwenyekiti wa chama hicho, Mussa Yusuph kutoka gazeti la Uhuru kuwa mshindi kwa kupata kura 23 dhidi ya wapinzani wake, Magnus Mahenge ambaye alipata kura 20, huku Daniel Mkate kutoka EATV akipata kura 19.

Aidha, alisema nafasi ya Makamu Mwenyekiti Katare Mbashiru kutoka Dailynews ameibuka mshindi kwa kupata kura za ndio 58 akiwa ni mgombea pekee wa nafasi hiyo.

"Nafasi ya Katibu Mkuu CPC, Benchine Bango mwandishi wa kujitegemea ameshinda kwa kupata kura 38, huku Blaya Moses akipata kura 25, nafasi ya Katibu Msaidizi Mussa Enock alikuwa mgombea pekee na amepata kura za ndiyo 59," alisema.

Kuhusu nafasi ya wajumbe, alisema waliochaguliwa ni Jasmine Shamwepu, Dotto Kwilasa na Amani Mmbando.

Akizungumza baada ya kutangazwa, Mwenyekiti wa CPC, Mussa Yusuph, aliwashukuru wanachama hao kwa kumchagua na kuahidi kushirikiana nao katika kukiletea maendeleo chama hicho.

"Ndugu wanachama wenzangu, imani yenu kubwa mlioionyesha kwangu, hilo ni deni ambalo ninapaswa kulilipa iwe kwa jasho, damu, machozi, mchana au usiku lazima niwatumikie kwani mimi kwenu sio kiongozi bali mtumishi wenu ninayepaswa kuwatumikia," alisema.

Naye Mwenyekiti Mstaafu wa CPC, Habel Chidawali, aliwapongeza viongozi waliochaguliwa na kuahidi kutoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha wanakidhi kiu ya wanachama hao.

# Watakaozidisha ujazo mpunga faini mil. 50/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, ameagiza kukamatwa na kutozwa faini ya kuanzia shilingi 100, 000 hadi milioni 50 kwa watu wote husu-san wafanyabiashara watakao-bainika wamezidisha ujazo kwe-nye maroba ya mpunga.

Mfune alitoa kauli hiyo mwis-honi mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya tatu ya mwaka 2019/2020 kilichofanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Rujewa, kwa ajili ya kujadili shughuli mbalim-bali za maendeleo zinazoendela katika halmashauri.

Alisema agizo hilo amelitoa muda mwafaka ambao ni msimu wa mavuno ya zao la mpunga, na kwamba kipindi hiki baadhi ya wafanyabiashara hukitumia kuwakandamiza wakulima kwa kuwalangua.

Alisema ili kudhibiti tabia hiyo, watakaobainika watatozwa faini kwa mujibu wa sheria za vi-pimo, zikiwamo za halmashauri kuanzia shilingi 200,000 hadi milioni moja.

"Tumeingia kwenye msimu wa mavuno ya mpunga, kuna watu wanajiona ni wajanja wa-natuletea maroba makubwa yenye ujazo wa zaidi ya kilo 100 na rangi sawa na maroba yali-yoruhusiwa... sisi hatuangalii rangi ya mifuko, tutaikagua na kwa wale wa-takaozidisha uzito ulioruhusiwa wata-pigwa faini na watachukuliwa hatua za kisheria kwa kushirikiana na wakala wa vipimo," alisema Mfune.

**Tumeingia kwenye msimu wa mavuno ya mpunga, kuna watu wanajiona ni wajanja wanatuletea maroba makubwa yenye ujazo wa zaidi ya kilo 100 na rangi sawa na maroba yaliyoruhusiwa... sisi hatuangalii rangi ya mifuko, tutaikagua na kwa wale watakaozidisha uzito uliorusi-wa watapigwa faini na watachukuliwa hatua za kisheria kwa kushirikiana na wakala wa vipimo**

Aidha, aliagiza kuchukuliwa hat-ua watakaobainika wanakwamisha zoezi la ukusanyaji mapato wilayani humo, na kuwaomba wazabuni ambao hawajawasilisha fedha za makusanyo kufanya haraka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hal-mashauri ya Wilaya hiyo, Kivuma Msan-gi, aliwaomba madiwani kuendelea kutoa ushirikiano kwa wataalamu ka-tika suala la ukusanyaji wa mapato.

Alisema hadi kufikia sasa mapato ya ndani yamefikia asilimia 81 na lengo kubwa kuvuka malengo waliyojiwekea.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mbeya Mjini, Afrey Msomba (kushoto), akiwaonyesha wanachama vifaa walivyopokea ili kujikinga na ugonjwa wa Covid- 19, ambavyo ni ndoo za maji na magaloni ya sabuni, vilivyotolewa na Taasisi ya Tulia Trust mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Kinamama lawamani utapiamlo kwa watoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wanawake mkoani Mbeya, wanadaiwa kuchangia tatizo la utapiamlo kwa watoto.

Wanalalamikiwa kuwa hali hiyo inatokana na kushindwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya juu ya namna ya ku-nyonyesha.

Hayo yalisemwa mwisho wa wiki na Ofisa Lishe wa Hos-pitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Charles Msigwa, ambapo alieleza kuwa mtoto asiponyonyeshwa maziwa ya mama kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo ana hatari kubwa ya kukosa virutubisho muhimu ambavyo vinahitajika kwa ajili ya ukuaji wake, hivyo kusababisha utapiamlo.

Alisema baadhi ya watoto wanaopimwa kliniki katika hospitali hiyo afya zao sio za kuridhisha, kutokana na wen-gine kudhoofu na wengine kuwa na tumbo kubwa.

Alisema miongoni mwa saba-bu zinazosababisha utapiamlo kwa watoto ni kinamama walio wengi kuwa na shughuli mbal-imbali za uzalishaji na ujasiria-mali, hivyo hushindwa kumaliza miezi sita wakihofia kukwami-sha kazi zao.

"Mtoto asiponyonyeshwa kwa miezi sita ya mwanzo anaweza kupata ugonjwa wa kwashakoo au utapiamlo, tumejitahidi kutoa elimu ya unyonyeshaji kwa kinamama, lakini wengine hawa-zingatii matokeo yake watoto wanapata maradhi," alisema Msigwa.

Aidha, Dk. Msigwa alisema kuwa zipo athari zitokanazo na mama kutomnyonyesha mtoto ikiwamo saratani ya matiti kwa sababu maziwa yanayotakiwa kutoka yanagandia ndani na kutengeneza mafuta.

Mmoja wa wanawake ku-toka Mtaa wa Juhudi jijini humo, Jenifer Kabuka, alisema kinachosababisha kuwaachisha maziwa watoto ni hali ngumu ya maisha, hivyo hulazimika kwenda mashambani au ku-fanya shughuli za ujasiriamali ili kupata fedha za kuendesha maisha yao.

Jenifer alisema kwa sababu ya kuwa na shughuli nyingi za kujiingizia kipato, watoto hu-nyweshwa uji, ambao umfanya mtoto kuacha kusumbua.

# Wanaowafanyia ukatili watoto, wanawake watangaziwa kiama

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya mkoani Mbeya, imeapa kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaojihusisha na vitendo vya mauaji, ubakaji, ulawiti dhidi ya wanawake na watoto.

Hatua hizo zitachukuliwa wakati huu ambapo shule zimefungwa na shughuli zinafanywa kwa tahadhari kubwa ili kujikinga na ugonjwa wa Covid-19.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Marryprisca Mahundi, aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe juu ya mikakati waliyoiweka katika kukabiliana na vitendo vya ukatili kipindi hiki cha mapambano dhidi vya Covid-19.

Alisema vitendo vya mauaji, ulawiti na ubakaji kwa wanawake na watoto vinahusishwa na imani za kishirikina kutoka kwa wachimbaji wa dhahabu ambao huamini kufanya hivyo kutawaletea utajiri na kupata madini mengi ya dhahabu.

Alisema Serikali ya Wilaya Chunya imejipanga vyema kukabiliana na vitendo hivyo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, madiwani na wananchi ambapo mpaka sasa vitendo hivyo vimeanza kupungua kwa sababu ya kuripotiwa na wahusika kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Katika kipindi cha mwaka 2019, matukio ya ubakaji, mauaji na ulawiti yaliripotiwa saba na kwa mwaka 2020 hadi kufikia Machi yalikuwa mawili, tunaamini ni hatua kubwa katika kukabiliana navyo tunaendelea kupambana ili kuhakikisha vinatokomea kabisa," alisema Marryprisca.

Alieleza kuwa mikakati waliyoipanga ili kutomeza vitendo hivyo ni kutoa elimu kwenye kata zote 20 za wilaya hiyo kuhusu athari za vitendo hivyo na kuachana na imani za kishirikina.

Hata hivyo, alilipongeza Jeshi la Polisi wilayani humo kwa utendaji kazi wake katika kupambana na vitendo hivyo kwa maelezo kuwa wanafuatilia na kuwakamata watuhumiwa wote wanaoripotiwa kuhusika na vitendo hivyo.

Katika taarifa yake hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwatahadharisha wale wote watakaohusika kuwapa mimba wanafunzi kipindi hiki cha corona kuwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria huku akiwasisitiza wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao.





# Mawaziri SMZ wammiminia sifa Balozi Augustine Mahiga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamemwelezea aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria marehemu Balozi Dk. Augustine Mahiga, kuwa mwanadiplomasia na mtumishi mwadilifu aliyefanya kazi zake huku akiwa muumini wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, Khamis Juma Mwalimu, alisema Tanzania imepoteza miongoni mwa viongozi wazalendo, mwadilifu na msomi ambaye amefanya kazi zake kwa maslahi ya taifa.

Mwalimu alisema alifahamiana na Balozi Mahiga baada yeye kuteuliwa kuongoza Wizara ya Katiba na Sheria Zanzibar na alijenga mahusiano makubwa na Balozi Mahiga ambao wizara zao majukumu yake yanafanana.

Alisema Balozi Mahiga aliishirikisha Wizara ya Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano yote ya kimataifa na kikanda inayohusu masuala ya wizara hizo mbili.

"Katika kipindi kifupi nilifuatana na naye katika mikutano mbalimbali ya kimataifa na kikanda inayohusu masuala ya wizara mbili kwa kujenga ushirikiano mkubwa," alisema.

Aidha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Haroun Ali Suleiman, alisema alifahamiana na Balozi Mahiga alipoteuliwa kuwa Waziri wa Ushirikiano wa Kimataifa na kikanda na kupata kufanya kazi naye kwa karibu.

Alisema alichomfahamu haraka kwamba Balozi Mahiga alikuwa muumini mkubwa wa Muungano na kuona kila pande zinashiriki vizuri katika masuala ya Muungano ikiwamo ushiriki wa mikutano ya kimataifa.

"Balozi Mahiga alikuwa akiongoza Wizara ya Mambo ya Nje ambayo ni taasisi ya Muungano, ambapo katika kipindi chote hicho aliwashirikisha vizuri mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya kimataifa na kikanda.

Naye Waziri wa Vijana, Michezo, Sanaa na Utamaduni, Balozi Ali Karume, alisema anamfahamu vizuri Balozi Mahiga ambapo katika nyakati tofauti walikuwa wakishirikiana kuiwakilisha Jamhuri ya Muungano katika mikutano mbalimbali ya kimataifa.

Karume alimwelezea Balozi Mahiga kama ni miongoni mwa wanadiplomasia mahiri wachache waliopo Afrika waliokuwa na uwezo katika maeneo mbalimbali.

"Balozi Mahiga ni miongoni mwa wanadiplomasia mahiri wenye sifa waliobobea katika masuala mbalimbali ya uhusiano wa kimataifa...nilifanya kazi naye vizuri wakati nikiiwakilisha Tanzania Marekani, Ubelgiji pamoja na Ujerumani hadi Italia," alisema.

Uwezo na umahiri wa marehemu Balozi Mahiga ulimfanya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wakati huo, Ban Ki Moon, kumteua kuwa mwakilishi wake maalumu mwaka 2010-2013 katika kuupatia ufumbuzi wa mgogoro wa kisiasa Somalia.



Naibu Waziri wa Elimu Zanzibar, Simai Mohamed Said (mwenye kofia), akiwa na Naibu Sheha wa Ubago Cheche, Said Ali Shaali, wakikagua na kufanya tathmini ya mafuriko ambayo yamewakumba wakazi wa shehia hiyo jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA.**

## Wazazi, walezi waombwa vita mimba shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWALIMU Mkuu wa Shule Sekondari Paje Wilaya ya Kusini Unguja, Abdallah Issa Makame, amesema wanahitaji nguvu za pamoja kati ya wazazi na walezi ili kupiga vita mimba za ututoni kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Akizungumza na Nipashe mwalimu mkuu huyo, alisema wamekuwa na bidii ya kuwaelimisha watoto hao pamoja na kuwakataza kufanya vitendo viovu, lakini wanavunjika moyo kutokana na baadhi ya wazee na walezi kutowapa ushirikiano.

Alisema katika miaka ya hivi karibuni kulijitokeza matukio matatu ya wanafunzi kupata ujauzito, ambapo kama waalimu wameyachukulia ni mengi na kuongeza kampeni ya kutoa elimu kwa wanafunzi hao.

Hata hivyo, alisema kuwa wamekuwa na utaratibu wa kuwapa ushauri nasaha wanafunzi hao kwa kuwapelekea watoa ushauri nasaha wa nje ili kuwafunza juu ya kujikinga na vitendo viovu ikiwamo kufanya ngono wenyewe kwa wenyewe.

Alisema juhudi hizo zinaonekana kutosaidia na wanapoona kuna watoto wamekuwa watukutu zaidi huwaita wazazi na walezi, lakini majibu wanayoyatoa yanawavunja moyo.

Aliwataka wazazi na walezi kujitahidi kuwalea watoto wao katika misingi iliyobora na waelewe kuwa wana jukumu la kuwafuatilia nyendo zao zote na sio kusema kuwa wameshindwa.

Jumla ya kesi nne za mimba kwa wanafunzi zimetokea shuleni hapo kutoka mwaka 2017 hadi 2020.

Alisema katika mimba hizo kesi tatu wanafunzi hao wamepata kutoka kwa wanaume wa nje na kesi moja ni mwanafunzi kwa mwanafunzi.

# Unyanyapaa waendelea waliopona corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UNYANYAPAA kwa waliopona corona umezidi kushika kasi, hali ambayo imesababisha baadhi ya waliopona kukosa huduma muhimu za kijamii.

Akizungumza na Nipashe, Halima Juma sio jina halisi, alisema bora maisha aliyokuwa akiishi katika kambi ya wagonjwa wa corona kuliko maisha anayoishi hivi sasa katika jamii.

Akieleza kwa masikitiko makubwa alisema kuwa baada ya kutoka hospitali alirejea nyumbani kwake na kukuta mita yake ya umeme haifanyi kazi na kukaa bila ya kuwa na umeme.

"Nilimpigia simu fundi aje anitengenezee mita yangu ili niweze kupata umeme alikataa kuja kwangu kisa kaambiwa na majirani kuwa mimi nina corona," alisema.

Aidha, alisema maisha ya uraiani yamekuwa na changamoto kubwa kwake kwa sababu hana msaada wowote anaoupata kutoka kwa ndugu na majirani na hulala na njaa kutokana na kukosa chakula.

Aliendelea kusimulia: "Jana nimelala na njaa, sina pesa wala chakula na hivi sasa nimetakiwa nikae ndani kwa muda wa siku 14 sina biashara yoyote ninayoifanya."

Halima ambaye awali kabla ya kupata ugonjwa huo alikuwa ni mfanyabiashara mama lishe, hivi sasa biashara yake imesita kutokana na kupata ugonjwa huo.

Alieleza kuwa maisha waliyokuwa wakiishi katika kambi ya wagonjwa wa corona yalikuwa ni nafuu kwake kwa sababu wanapata chakula kizuri, tena kwa wakati.

"Tunapongeza sana Rais Wetu, Dk. Ali Mohamed Shein kwa kweli tulikuwa tunashughulikiwa vizuri wala hatukuwa na msongo wa mawazo wakati tulipokuwa huko," alisema.

Alieleza kuwa baada ya kurejea nyumbani kwake amekuwa na msongo wa mawazo, huku akiwaza atakula nini wakati hana fedha na wala hafanyi biashara.

Aliiomba serikali kuwapatia msaada angalau wa chakula kutokana na hali zao za kiuchumi hivi sasa ni ngumu na hana mtaji wowote ambao utamwezesha kufanya biashara baada ya kumaliza kukaa karantini.

Asha Seif sio jina lake halisi, na yeye ni miongoni mwa waliopona corona, alisema kuwa ameamua kuhama nyumba anayoishi kutokana na kunyanyapaliwa na majirani zake.

"Mtaa huu nahama maana uso wangu sina pa kuweka naona nitakufa kwa msongo wa mawazo maana nanyanyapaliwa mimi, mume wangu hadi watoto wangu," alisema.

Alieleza kuwa amejenga nyumba nyingine nje ya Mkoa wa Mjini Magharibi, ingawa hajakamilisha ujenzi, lakini ameamua kwenda kuishi.

"Mtaa ninaoenda kuhamia ni mgeni hivyo watu hawanijui kama nilipata corona," alieleza.

Naye Waziri wa Afya, Hamad Rashid Muhammed, ameitaka jamii kuacha kuwanyanyapaa waliopona corona kwani bado wanahitaji msaada wao.

Alisema mgonjwa wa corona ni sawa na mgonjwa mwingine, hivyo ni vyema kumpa msaada ili aweze kupata mahitaji muhimu.

"Ni kweli upo unyanyapaa mkubwa kwa jamii kwa waliopona corona... kwa kweli jambo hili halipendezi hata kidogo, maana huu ugonjwa hauna mtu maalum muhimu ni kuchukua tahadhari na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya," alisema Hamad.

# Wanaofuata uvumi mitandao kijamii matumizi dawa waonywa

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, imetoa ufafanuzi na kuwaonya wananchi kutotumia dawa kiholela kwa kufuata uvumi unaosambaa katika mitandao ya kijamii.

Uvumi huo unahusu uwapo wa baadhi ya dawa zinazodaiwa kuwa na uwezo wa kuzuia au kutibu ugonjwa wa homa ya corona.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makundi, alisema hivi karibuni kumekuwapo na taarifa za kutumika kwa dawa hizo, hivyo kusababisha baadhi ya dawa za kutibu magonjwa yaliyozoeleka kutumika kiholela miongoni mwa wananchi.

Alisema taarifa hizo zinazosambaa katika mitandao ya kijamii zilidai kuwa dawa za Azithromycin, Aspirin, Prednisolone, Zinc, Asscorbic Acid (Vitamini C) na baadhi ya dawa za kupunguza makali ya Ukimwi (ARV), zinaweza kuzuia au kutibu ugonjwa wa corona.

"Wizara inapenda kuufahamisha umma kuwa mpaka sasa hakuna dawa ya kuzuia au kutibu corona, dawa zote hutumika kwa kuzingatia mwongozo wa daktari. Dawa kama Azithromycin hutumika kutibu magonjwa mbalimbali yakiwamo magonjwa ya homa ya mapafu itokanayo na bacteria na siyo virusi," alisema Prof. Makundi.

Aliongeza: Dawa ya Asprin hutumika kwa ajili ya maumivu, homa, na wagonjwa wa moyo kwa maelekezo maalum ya daktari. Prednisolone kwa magonjwa ya ngozi, pumu n.k, na dawa za ARV kwa ajili ya wagonjwa wenye virusi vya Ukimwi.

Prof. Makundi alisema matumizi holela ya dawa hizo yanaweza kusababisha madhara makubwa ikiwamo usugu wa dawa na hivyo kushindwa kutibu tena magonjwa yanayotokana na bakteria.

"Dawa zingine zina madhara makubwa, kwa mfano Aspirin huleta vidonda vya tumbo na kutokwa na damu. Prednisolone huleta madhara ya kupandisha sukari na kuvimba baadhi ya sehemu za mwili mzima," alisema Prof. Makundi.

Alisema dawa nyingine kama Ascorbic Acid na Zinc ni virutubisho ambavyo vipo kwenye matunda mbalimbali nchini na hutumika tu kama mbadala kwa mgonjwa asiye na uwezo wa kula matunda kwa kiwango kinachotakiwa.

"Kama hizi dawa zingekuwa zinatibu au kuzuia hili tatizo, basi vingekuwa vimetumika sana huko Uchina, Ulaya na Marekani maana huko ndiko zinazalishwa kwa wingi," alisema Prof. Makundi.

Alisema wizara inawasihi wananchi kupuuza taarifa zisizo za kweli na kuisikiliza na kupata taarifa sahihi kutoka kwake.

"Hadi sasa hakuna dawa ya kutibu au kuzuia ugonjwa huu, ila kuna dawa zinazosaidia kutibu mgonjwa akiwa katika hatua fulani, kwa ushauri wa daktari na hakuna uthibitisho wa dawa hizi kuwa zinaweza kuzuia au kutibu corona," alisema Prof. Makundi na kuongeza:

"Dawa zote lazima ziandikwe na daktari na si kila mtu atumie kwa jinsi anavyojisikia, wananchi wanaojihisi dalili zozote za ugonjwa wa COVID-19 wanashauriwa kutoa taarifa kwa kupitia simu namna 199 bila malipo."

Alilitaka Baraza la Famasia kusimamia kikamilifu uuzwaji holela wa dawa katika maduka ya dawa ili kuzuia usugu wa dawa kwa Watanzania.

Kuhusu maiti kuzikwa usiku, Prof. Makundi alisema hakuna sababu ya maiti za watu waliofariki kwa ugonjwa wowote ule kuzikwa usiku au gizani katika kipindi hiki.




Ofisa Usalama Mahali Pakazi wa kampuni ya Asas mkoani Iringa, Cosmas Charles (kushoto), akimkabidhi Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa, Dk. Alfred Mwakalebela, mashine ya kutakasa mwili jana kwa ajili ya kujikinga na virusi vya corona. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Wajumbe wa NEC watembelea vituo daftari

**Na Maulid Mmbaga**

KATIKA utekelezaji wa uboreshaji wa daftari la mpigakura awamu ya pili kuanza Mei 2, mwaka huu, wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wamefanya ziara za kutembelea vituo mbalimbali kuhakikisha mchakato huo unatekelezwa kwa ufanisi.

Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, jana alitembelea vituo mbalimbali vya wapigakura katika halmashauri za manispaa za Kinondoni, Temeke na Ilala mkoani Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo Jaji Kaijage aliambatana na Mkurugenzi Msaidizi wa Habari, Dk. Cosmas Mwaisobwa, kuangalia mwenendo wa uboreshaji wa taarifa katika daftari hilo.

"Katika kata zote ambazo tumezitembelea, nimeridhishwa na mwenendo wa zoezi hili ambapo kila sehemu wameweka utaratibu maalumu wa kujikinga na corona... pia wananchi wahakiki taarifa zao kabla zoezi halijafungwa," alisema Jaji Kaijage.

Pamoja na kuridhishwa na taratibu za kujikinga na COVID-19, pia Jaji Kaijage aliwasisitiza watendaji wote kuzingatia taratibu, sheria na maelekezo ya NEC.

Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Mahera, naye alifanya ziara ya kutembelea vituo vya kuandikisha wapigakura katika baadhi ya maeneo jijini Dodoma, ambapo alitoa wito wananchi kizingatia tahadhari dhidi ya corona.

"Zoezi hili la kuandikisha wapigakura litafanyika kwa siku tatu kuanzia Mei 2 hadi 4, hivyo... natoa rai kwa washiriki wote kuhakikisha wanazingatia taratibu za kujikinga na ugonjwa wa COVID-19 ili kulinda afya zenu," alisema.

Mjumbe wa Tume hiyo, Jaji Thomas Mihayo, alifanya ziara katika vituo vya Halmashauri ya Chamwino Ikulu na Bwigiri mkoani Dodoma, ambapo alisisitiza uzingatiaji wa tahadhari za kiafya dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Makamu mwenyekiti wa tume hiyo, Mbarouk Salim Mbarouk, alitembelea vituo katika wilaya za Wete, Micheweni na Chakechake kisiwani Pemba, alieleza na aliridhishwa na utekelezaji.

# Askofu Katoliki ataka utulivu mlipuko wa corona

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

ASKOFU wa Jimbo Katoliki la Moshi mkoani Kilimanjaro, Ludovick Minde, amesisitiza waumini wa kanisa hilo na Watanzania kwa ujumla kuwa na utulivu katika kipindi hiki taifa linakabiliwa na janga la virusi vya corona.

Aliyasema hayo jana Katika Kanisa la Mtakatifu Karoli Lwanga mjini Kahama, baada ya kuwaapisha viongozi wa kamati tendaji ya Jimbo Katoliki la Kahama pamoja na viongozi wa kamati tendaji za parokia katika jimbo hilo.

Askofu Minde ambaye ni Askofu Msimamizi wa Kitume katika jimbo Katoliki la Kahama, alisema wakati huu ni wa kujiweka mbele za Mwenyezi Mungu, kwa sala na maombi, huku akiipongeza serikali kwa kuruhusu madhehebu ya dini yaendelee kusali, na kwamba huo ni upendeleo wa pekee unaotoka kwa Mwenyezi Mungu.

Katika hatua nyingine, Askofu Minde aliwataka waumini walei kuendelea kushirikiana na mapadri katika kulijenga kanisa la Mungu, huku akiwataka mapadre nao wazidi kushirikiana na viongozi hao pamoja na waumini bila ubaguzi.

Paroko wa Parokia ya Kahama Mjini, Jimbo Katoliki la Kahama, Padre Salvatore Guerrer, aliwataka Wakatoliki wilayani Kahama kutambua kuwa Yesu Kristo ndiye mwokozi wa maisha yao ya kila siku kwa, kuwa ndiye mchungaji mwema, hivyo ni vyema kuifuata sauti yake.

Alisema Wakatoliki wana wajibu wa kutambua kuwa wao ni kondoo wa Yesu Kristo, na kwamba wanapaswa kuwa karibu na Yesu Kristo kwa kuyafuata mafundisho kwa utii na unyenyekevu katika sala, maombi na ibada.

Katika hatua nyingine, Padre Salvatore aliwataka waumini kuendelea kuwaombea mapadre na watawa ili waendelee kuwa wachungaji wema katika kuliongoza Kanisa Katoliki popote Duniani ikiwamo kuwalea watoto na vijana katika miito ya utumishi ndani ya kanisa.

Naye Katibu wa Parokia ya Kahama Mjini, Francis Ntelya, aliwakumbusha waumini kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya virusi vya corona, na kwamba kanisa hilo limeweka utaratibu wa kuvaa barakoa wakati wa ibada na misa zote kama tahadhari.

## HABARI KIMATAIFA

# Mataifa Afrika kutumia dawa kutoka Madagasca

**ANTANANARIVO,** Madagasca

WAKATI wanasayansi duniani wakihangaika kupata chanjo na tiba ya ugonjwa wa virusi vya corona, hivi karibuni Rais wa Madagascar, Andry Rajoelina, alizindua dawa ya mitishamba inayotibu ugonjwa wa corona.

Kwa muda wa wiki mbili sasa, Rais Andry Rajoelina (pichani) amekuwa akifanya mazungumzo na viongozi wenzake wa nchi za Afrika.

Ndege ya nchi ya Equatorial Guinea iliwasili Jumatano alasiri jijini Antananarivo ili kuweza kubeba tani 1.5 za dawa hiyo.

Wakati huo huo, ndege nyingine kutoka Guinea-Bissau inatarajiwa kutua muda wowote kwenye uwanja wa Antananarivo, Madagascar.



Hata hivyo, Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema kuwa hakuna ushahidi wa tiba ya ugonjwa wa corona ambayo imethibitishwa licha ya Rajoelina kutangaza dawa yake.

Nayo Taasisi ya taifa ya tiba nchini Madagascar (Anamem) pia imeonyesha wasiwasi wake juu ya ufanisi wa dawa hiyo inayoelezewa na Rais Andry Rajoelina kama yenye uwezo wa kuzuwia na kupona corona.

Wakati wa mazungumzo yake na Andry Rajoelina, Umaro Sissoco Embalo, Rais wa Guinea-Bissau alisema kwamba anaweza kuchukuwa dawa hiyo kutoka Madagascar na kuisambaza kwa wanachama wa Jumuiya ya Kiuchumi ya nchi za Magharibi mwa Afrika, ECOWAS, yaani nchi 15.

Mkurugenzi wa ofisi ya Rais wa Madagascar, Lova Hasinirina Ranoromaro alisema dawa hiyo tayari imeshakubaliwa na Senegal na Togo. **RFI**

# Hispania yaruhusu wananchi kutoka nje

**MADRID,** Hispania

WAKAZI wa Hispania juzi waliingia mitaani kufanya mazoezi ya kukimbia, kupanda baiskeli na michezo mingine kwa mara ya kwanza, kufuatia siku 48 za kulazimika kubakia majumbani mwao.

Wakati huo huo, baadhi ya mataifa ya Ulaya kwa tahadhari yalilegeza vizuwizi vya kutoka nje, wakati Urusi na Ujerumani zimeripoti ongezeko la maambukizi.

Wakati serikali zikitafakari kuondoa vizuwizi vya kuwataka wananchi kubakia majumbani ili kuanzisha tena uchumi wao, maofisa nchini Marekani wameleta matumaini kiasi kwa kuidhinisha dawa ya majaribio ili itumike kwa wagonjwa wa virusi vya corona.

**Baada ya wiki kadhaa za kufungiwa, nilikuwa nahitaji sana kutembea nje, kukimbia, na kuona dunia, jana nilikuwa kama mtoto katika mkesha wa Krismasi.**

Uamuzi huo ulikuwa wa hivi karibuni kabisa katika hatua za dunia kutafuta dawa na chanjo kwa ajili ya virusi vya corona, ambavyo vimesababisha nusu ya watu dunia kuwamo katika vizuwizi vya kutoka nje.

Virusi vya corona hadi sasa vimewaua zaidi ya watu 242,000 duniani kote, kwa mujibu wa idadi iliyowekwa pamoja na Shirika la Habari la AFP, na walioambukizwa wanafikia milioni 3.4 tangu kuzuka mara ya kwanza virusi hivyo nchini China mwishoni mwa mwaka jana.

Kukiwa na ishara kwamba janga hili linapungua kasi katika mataifa yale yaliyoathirika zaidi, mataifa ya Ulaya pamoja na baadhi ya sehemu za Marekani yameanza kuondoa vizuwizi kujaribu kurejesha hali ya maisha kuwa ya kawaida katika uchumi ambao ulioathirika kutokana na wiki kadhaa za kufungwa.

Kuanzia mji wa Madrid hadi Mallorca, Wahispania walimiminika mitaani baada ya kuruhusiwa kufanya mazoezi na kutembea huru nje baada ya serikali kulegeza wiki saba za udhibiti katika nchi hiyo.

"Baada ya wiki kadhaa za kufungiwa, nilikuwa nahitaji sana kutembea nje, kukimbia, na kuona dunia, jana nilikuwa kama mtoto katika mkesha wa Krismasi," alisema Marcos Abeytau ambaye ni mshauri wa masuala ya fedha mjini Madrid.

Hispania, Ujerumani, Austria na mataifa ya Scandinavia yameanza kulegeza vikwazo vya kuwazuwia watu kutoka majumbani, wakati kesi za virusi vya corona zikipungua licha ya kuwa hatua za watu kukaa mbalimbali zitaendelea. **DW**



Mtoto akipanda baiskeli karibu na mfanyakazi anayeweka dawa katika maeneo ya nje ya mjini Madrid kuua virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**



# Kim Jong-un aonekana hadharani

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un (pichani) ameonekana hadharani kwa mara ya kwanza baada ya siku 20, vyombo vya habari vya Korea Kaskazini vimesema.

Shirika la habari la KCNA limeripoti kuwa kiongozi huyo wa Korea Kaskazini alionekana alikata utepe katika ufunguzi wa kiwanda cha mbolea.

Lilieleza kuwa wananchi waliojitokeza kwenye uzinduzi wa kiwanda hicho walimshangilia kwa shangwe kubwa alipojitokeza siku ya Ijumaa.

Taarifa za kuonekana kwake kwa mara ya kwanza tangu alipoonekana katika tukio kwenye vyombo vya habari vya taifa hilo, Aprili, 12 zinakuja huku kukiwa na tetesi duniani kuhusu afya yake.

Vyombo vya habari baadaye vilitangaza picha ambazo zilionyesha Kim akikata utepe nje ya kiwanda. Alipoulizwa kuhusu taarifa za kuonekana kwa Kim, Rais wa Marekani, Donald Trump aliwaambia waandishi wa habari kuwa asingetaka kuzungumzia lolote juu ya taarifa hizo.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Taifa- Korean Central News Agency (KCNA), Kim aliambatana na maofisa wa ngazi ya juu wa Korea Kaskazini, mkiwamo dada yake Kim Yo Jong.

Taarifa zaidi zinaeleza kwamba kiongozi huyo alikata utepe katika sherehe iliyofanyika katika kiwanda, katika Jimbo la Kaskazini mwa nchi la Pyongyang.

Kim alisema kuwa amefurahishwa na mfumo wa uzalishaji wa kiwanda na akakisifu kwa kuchangia katika maendeleo ya viwanda vya kemikali na uzalishaji wa chakula.

Tetesi kuhusu afya ya Kim zilianza baada ya kukosa katika sherehe za maadhimisho ya siku ya kuzaliwa ya babu yake, muasisi wa taifa Kim Il Sung Aprili, 15.

Kumbukumbu hiyo ni moja ya matukio makubwa katika kalenda ya Korea Kaskazini, na Kim kwa kawaida huadhimisha siku hii kwa kutembelea katika eneo la makumbusho yenye mnara ambako babu yake amezikwa. Kim hajawahi kukosa kuhudhuria tukio hili.

Madai kuhusu kuugua kwa Kim, yaliandikwa katika tovuti ya muasisi wa Korea Kaskazini.

Chanzo cha habari ambacho hakikutaka kufahamika kiliiambia Daily NK kuwa "wana taarifa kuhusu matatizo yake ya kiafya tangu mwaka jana mwezi Agosti, lakini tatizo limezidi kuwa kubwa baada ya kurudia kutembelea mlima Paektu". **BBC**



# NEYMAR ANAWEZA KUMPIKU MESSI, RONALDO - EMERY

**PARIS,** Ufaransa

UNAI Emery anaamini kwamba, Neymar ana uwezo wa kuwapiku Lionel Messi na Cristiano Ronaldo kuwa mchezaji bora duniani.

Kocha huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain alifanya kazi na Neymar kwa msimu wake wa kwanza kucheza Ufaransa baada ya nyota huyo wa Brazil kutua hapo kwa dau la euro milioni 222 kutoka Barcelona mwaka 2017.

Raia huyo wa Hispania ambaye aliondoka pale PSG mwaka 2018 na kwenda kuwa kocha wa Arsenal, alifurahia wakati aliokuwa na Neymar na ameendelea kuwa na imani juu ya kiwango na uwezo wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

"Nilikuwa na mwaka wa kuvutia na yeye," alisema Emery katika mahojiano yake kupitia Instagram na kocha wa Granada, Diego Martinez, ambaye alikuwa msaidizi wake pale Sevilla.

"Nilijifunza vingi sana wakati nikimwangalia mazoezini na kwenye mechi.

"Neymar ana kipaji kipo ndani yake, lakini ana uwezo na ubora wa kiwango cha daraja la juu kabisa.

"Nafikiri ana nafasi ya kuchukua nafasi ya Messi na Cristiano Ronaldo na kuwa mchezaji bora duniani, na ana muda wa kufanya hivyo."

Neymar ameshinda mataji sita katika misimu yake mitatu na PSG, likiwamo la Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kila mwaka.

# Marcelo hataki kuondoka Real Madrid

**MADRID,** Hispania

BEKI wa pembeni wa Real Madrid, Marcelo amesisitiza hataki kuondoka kwa miamba hao wa LaLiga wakati uvumi ukimhusisha na Juventus.

Raia huyo wa Brazil amekuwa akihusishwa kuondoka hapo Madrid, ambako amefurahia kipindi kizuri cha mafanikio tangu alipowasili akitokea Fluminense mwaka 2007.

Lakini Marcelo mwenye umri wa miaka 31, hana mpango wa kuondoka hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu, na anahisi pia Madrid wanamtaka abaki.

"Sitaki kuondoka na sidhani kama Madrid wataniacha niondoke," amemwambia Fabio Cannavaro wakati wa mahojiano live kupitia Instagram.

"Nina furaha kubwa hapa. Tangu nimekuja hapa na familia yangu, umekuwa wakati wa kuvutia sana.

"Kwa uhakika sijui kama kweli Juve wanataka nisaini kwao."

Marcelo ameendelea kuhusishwa na mpango wa kutakiwa Juventus, klabu ambayo anacheza mchezaji mwenzake wa zamani, Cristiano Ronaldo aliyejiunga nao mwaka 2018.





# *Ayala awachambua Maradona na Messi*

**BUENOS AIRES,** Argentina

DIEGO Maradona alikuwa na "kipaji halisi" na Lionel Messi ana "kasi ya Gonzales", kwa mujibu wa kocha msaidizi wa timu ya Taifa ya Argentina, Roberto Ayala.

Ayala alicheza pamoja na Maradona wakati akianza soka na baadaye akacheza na Messi.

Mlinzi huyo wa kati wa zamani wa Napoli, Milan na Valencia anaamini wachezaji hao ni watu wawili tofauti kabisa katika staili ya uchezaji, lakini anajisikia fahari kwamba ni wachezaji bora wanaotoka Argentina.

"Nilicheza na wote wawili, nilicheza na Diego wakati naanza hatua ya kwanza. Ni miamba wawili wa soka duniani, na wakati Messi atakapostaafu atakumbukwa sana," alisema Ayala akiiambia FOX Sports.

Kushindwa kwa Messi kubeba taji la kimataifa na timu ya Taifa ya Argentina mara kwa mara kumemfanya alinganishwe na Maradona, ambaye alitwaa Kombe la Dunia mwaka 1986.

Nyota wa Barcelona, Messi alipoteza katika fainali nne tofauti - tatu kwenye Copa America na moja kwenye Kombe la Dunia mwaka 2014, lakini Ayala anajiamini anaweza kupata mafanikio na Argentina.

# Ancelotti awatoa hofu Milan kwa kocha mgeni

**MILAN,** Italia

KOCHA wa zamani wa AC Milan, Carlo Ancelotti amesema mashabiki wa Rossoneri hao hawatakiwi kuwa na hofu kuhusu kuja kwa kocha wa kigeni, wakati uvumi ukienea kwamba, Rangnick anaweza kupewa mikoba hiyo.

Kocha mwenye uzoefu, Rangnick ambaye ni mkuu wa maendeleo ya soka kwa Kampuni ya Red Bull GmbH –inayoimiliki klabu ya RB Leipzig ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 61, amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa Milan, ambao kwa sasa wananolewa na kocha, Stefano Pioli.

Rossoneri wakati Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ikisimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona ilikuwa ipo nafasi ya saba kwenye msimamo na imekuwa na msimu mgumu kwao.

Ancelotti aliiongoza Milan kushinda mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Serie A, msimu wa 2001-09 wakati akiwa pale San Siro.

Sasa akiwa ndio kocha mkuu wa Everton, Ancelotti anaona hakuna sababu kwa nini kocha ajaye wa Milan hatakiwi kutoka nje ya Italia.





# TER STEGEN AELEZEA FURAHA KUCHEZA BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

GOLIKIPA wa Barcelona, Marc-Andre ter Stegen amesisitiza "ana furaha sana" hapo kwa mabingwa wa LaLiga, licha ya mazungumzo yake ya kuongeza mkataba mpya kusimama.

Mkataba wa sasa Ter Stegen unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22 na golikipa huyo raia wa Ujerumani amekuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich ambao wana mashaka na majaliwa ya Manuel Neuer.

Licha ya kuwa na maswali kuhusu majaliwa yake, Ter Stegen amesema sasa si muda wa kujadili kuhusu mkataba mpya kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Tayari tulishafanya majadiliano kwa mara ya kwanza," alisema Ter Stegen wakati wa mahojiano mubashara kupitia mtandao wa Instagram. "Lakini kama nilivyosema, tumesimama kwanza. Kuna vitu vingi zaidi muhimu. "Nina furaha kubwa hapa hali ya hapa ni nzuri na timu inafanya vizuri. Nini zaidi ninachotaka?"

Ter Stegen alijiunga na Barca akitokea kwa miamba wa Bundesliga, Monchengladbach mwaka 2014.

Tangu alipowasili pale Camp Nou, kipa huyo mwenye umri wa miaka 28 ameshinda mataji manne ya LaLiga pamoja na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Barca walikuwa wanaongoza msimamo wa ligi kwa pointi mbili dhidi ya wapinzani wao, Real Madrid baada ya mechi 27 wakati LaLiga ilipo-simamishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 Machi mwaka huu.

# *Adams ahofia Aubameyang kuuzwa*

**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang anatakiwa kuondoka Arsenal wakati wa dirisha la usajili kwa sababu imekuwa klabu ya kuuza wachezaji, nahodha wa zamani wa 'Washikabunduki' hao, Tony Adams amesema.

Ni mshambuliaji wa Leicester City pekee, Jamie Vardy, mwenye mabao 19, ambaye amefunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu msimu wa 2019-20 zaidi ya Aubameyang, ambaye alifunga 22 msimu uliopita na kuwa miongoni mwa wachezaji watatu walioshinda Kiatu cha Dhahabu.

Kiwango cha mshambuliaji huyo kimezivutia klabu kama Manchester United, Real Madrid na Paris Saint-Germain na zitajaribu kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 ili aondoke hapo London wakati wa dirisha la usajili litakapofunguliwa.

Alexis Sanchez, Alex Oxlade-Chamberlain na Robin van Persie ni miongoni mwa wachezaji waliondoka katika misimu ya hivi karibuni, na Adams anahofu Aubameyang, ambaye mkataba wake anamalizika msimu ujao, anaweza kufuata nyayo.

"Inawezekana kabisa, anaweza kuondoka," alisema Adams akiiambia Sky Sports.

"Nilipenda msimamo wa Arsene Wenger, kwamba hakuna mchezaji mkubwa kuliko klabu, na aliwauza wachezaji pale alipoona inahitajika kufanya hivyo kwa sababu ya kuongeza nguvu ya fedha kwa klabu.

"Alikuwa makini na hilo na ndio maana alikuwa akifuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kila mwaka, lakini kulikuwa na tatizo la kuwa klabu inayouza wachezaji bora.

"Kama ningekuwa kocha, ningesema, 'msimuuze Aubameyang kwa bei yoyote, tunahitaji kutengeneza timu, kuwapandisha wachezaji kutoka kwenye akademi na kuwabakiza wachezaji wetu bora'."

Adams alikumbushia enzi zake klabuni hapo akiwa na wachezaji wakali kama, Thierry Henry, Dennis Bergkamp na Patrick Vieira namna ambavyo walishikama.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE BRUYNE: FEDHA ZINAIRUDISHA EPL

## Hakuna anayependa kucheza bila mashabiki, lakini kama msimu hautamalizika, utasababisha...

**MANCHESTER,** England

KEVIN De Bruyne anaamini umuhimu wa kifedha ndio sababu itakayolazimisha Ligi Kuu ya England kumalizwa katika msimu wa 2019-20.

**Ripoti kutoka nchini England zimebainisha kuwa Juni 8, mwaka huu ligi hiyo itaendelea ikichezwa bila mashabiki kwa ajili ya kumalizia msimu.**

Wawakilishi wa klabu za England walikutana Ijumaa kujadiliana mpango waliouita 'Mradi wa kuanza tena', ikiwamo kuangalia usalama wa kiafya kwa kuwapima wachezaji wote, ili kupunguza hatari kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Nyota wa Manchester City, De Bruyne anatarajiwa kuanza mazoezi katikati ya mwezi huu, hata kama kucheza mechi bila mashabiki hakutamvutia yeye.

"Hisia zangu zinaniambia pengine tutaanza tena mazoezi kwa kipindi cha wiki mbili," alisema akiiambia HLN. "Serikali inataka kuanza tena kadiri inavyowezekana ili kuwapa watu kitu fulani.

"Kila kitu kitamalizika bila mashabiki, nafikiri. Kwa hakika kabisa hili halimvutii kila mmoja, lakini msimu huu utamalizika.

"Suala la kifedha ni muhimu sana kwenye Ligi Kuu ya England. Kama msimu hautamalizika, utasababisha matatizo makubwa."

Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, na ile ya Uholanzi, Eredivisie, zimefuta msimu wao, ingawa Ligi Kuu ya England sasa ipo pamoja na ya Ujerumani, Bundesliga, Hispania, LaLiga, na Italia maarufu Serie A, ambapo zote zinapanga kuendelea ili kukamilisha msimu.

Mshambuliaji wa City, Sergio Aguero aliiambia El Chiringuito wiki hii kwamba wachezaji wengi "wanaogopa" kurudi kwenye ligi kwa sababu ya hatari wanazoweza kuzisababishia familia zao, kitu ambacho De Bruyne - ambaye anatarajia mtoto wake wa tatu na mkewe - anakielewa.

"Kila mmoja atapimwa wakati tutakapoanza tena kucheza," alisema.

"Sidhani kama (wachezaji) wanaogopa kwa ajili yao wenyewe, lakini ni kwa sababu ya familia zao. Na hilo ndio tatizo kubwa kwa watu."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alikuwa na msimu binafsi wa kuvutia kabla ya ligi hiyo kisimama.

Alifunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho 16 kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku kiwango chake ndicho kilichoipa ushindi Man City wa 2-1 dhidi ya Real Madrid kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa hatua ya 16, michuano ambayo bado haijamalizika.

## ZISIKUPITE

### ROMA WAMTAKA SANCHEZ

KLABU ya AS Roma inataka kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Chile, Alexis Sanchez, 31, kwa mkopo. Kwa sasa anacheza pale Inter Milan, kwa mkopo akitokea Manchester United. ***(Sky Sport)***

### POCHETTION AMTAKA COUTINHO

WINGA wa Bayern Munich na Brazil, Philippe Coutinho, 27, atakuwa kwenye rada za Newcastle kama Mauricio Pochettino atakuwa kocha mpya. ***(Mirror)***

### MADRID KUUZA NYOTA 5

KLABU ya Real Madrid inapanga kuwauza angalau wachezaji watano kipindi kinachokuja cha majira ya joto, akiwamo winga wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 30. ***(AS)***

### PSG YAMUWANIA NDIDI

KIUNGO wa Leicester na timu ya Taifa ya Nigeria, Wilfred Ndidi mwenye umri wa miaka 23, anawaniwa na klabu ya Paris St-Germain ya Ufaransa. ***(ESPN)***

### WEST HAM KWA JOVIC

NEWCASTLE United na West Ham ni miongoni kwa klabu za Ligi Kuu England zinazomuwania mshambuliaji wa Real Madrid na Serbia, Luka Jovic, 22. ***(90min)***

### LEICESTER 'YAIBIPU' ARSENAL

KLABU ya Leicester itatuma ofa ya kumsajili mlinzi wa kushoto wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 22, kama beki wao wa kushoto wa kimataifa wa England, Ben Chilwell mwenye miaka 23, atauzwa. ***(Express)***

### BARCA KUMUUZA SUAREZ

BARCELONA inaweza kumuuza mshambuliaji wake wa kimataifa wa Uruguay, Luis Suarez kipindi cha majira ya joto kinachokuja, huku klabu kadhaa za Ligi ya Marekani zikiripotiwa kumuwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 33. ***(Marca)***

### LINGARD AGOMBEWA EPL

KLABU za Newcastle, Everton, West Ham na Leicester zote zinamfuatilia kwa karibu kiungo wa Manchester United na timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 27. ***(90min)***

### DE BRUYNE KUONDOKA CITY

KIUNGO wa kimataifa wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 28, amedokeza anaweza kuondoka Manchester City kama adhabu yao ya kufungiwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiendelea. ***(HLN)***

### SMALLING KUBAKI ROMA

AS Roma inataka kumbakiza mlinzi wa Manchester United na timu ya Taifa ya England, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, ambaye anacheza hapo kwa mkopo, angalau kwa msimu mmoja zaidi, amesema kocha, Paulo Fonseca. ***(ESPN)***

### LILLE KUMUUZA OSIMHEN

KLABU ya Lille ya Ufaransa, imepokea ofa ya euro milioni 85 na klabu ambayo haijatajwa jina kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji wake wa kimataifa wa Nigeria, Victor Osimhen. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amekuwa akiwaniwa na Liverpool. ***(Telefoot)***

HABARI MICHEZO

## Pamba wagawa vifaa vya corona

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

TIMU ya mpira ya Pamba Sport Club ya mkoani Mwanza kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, Stanslaus Mabula, wamegawa msaada wa vifaa vya kunawia mikono kwa uongozi wa Soko Kuu la mkoa huo lililopo Mbugani.

Vifaa hivyo vya kunawia mikono vyenye uwezo wa kubeba lita za ujazo 800, vimetolewa kwa ajili ya kusaidia kudhibiti na kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19) ili kutumiwa na wafanyabiashara na watu wanaoenda kupata huduma sokoni hapo.

Akikabidhi vifaa hivyo, Mwenyekiti wa Pamba Sport Club, Aleem Alibhai, alisema klabu hiyo kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, Stanslaus Mabula wametoa msaada huo kutokana na ombi maalumu la uongozi wa soko hilo.

Kwa upande wake mwakilishi wa Mabula, Florah Magabe, alisema mbunge huyo anawathamini wananchi wake ambao ni zaidi ya 350,000, huku ikiwa ni jimbo na wilaya pekee mkoani hapa inayohudumia takriban watu 700,000 hadi milioni moja kutoka mikoa ya jirani ya Kanda ya Ziwa pamoja na nchi za maziwa makuu wanaokuja kupata huduma za kijamii.

Alisema Nyamagana ndio eneo lenye msongamano mkubwa wa watu na uhitaji mkubwa wa vifaa vya kunawia mikono pamoja na vitakasa mikono kipindi hiki taifa likikabiliana na corona.

Naye Mwenyekiti wa Soko Kuu Mwanza, Hamadi Nchora alishukuru kwa msaada huo, huku akiomba taasisi zingine zijitokeze kuwasaidia vifaa vya kunawia na vitakasa mikono ili kudhibiti maambukizi kwa wafanyabiashara na wananchi wanaopata huduma sokoni hapo.

## Prisons kuanika dirisha la usajili

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa benchi la ufundi la klabu ya Tanzania Prisons umesema wiki ijayo utatoa utaratibu mzima wa usajili wa wachezaji wanaowahitaji kwa msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Adolph Richard, alisema mpaka kufikia wiki ijayo atatoa mikakati yake yote kuelekea dirisha la usajili lijalo.

"Wiki ijayo nitasema msimamo wangu wa usajili pamoja na kutaja idadi kuu ili msimu ujao turudi kwa kasi," alisema Adolph.

Alisema wanawasiliana na wachezaji wake kila mara ili kutaka kufahamu maendeleo yao, katika kipindi hiki cha mapumziko. Alikiri kuridhishwa na mwenendo wa wachezaji wake wanaoufanya kwa kufuata kwa makini programu alizowapa pamoja na kuwataka waongeze juhudi zaidi.

"Wananipa matumaini wapo makini na mazoezi wanajua huwa sitaki masihara katika kazi, mtu akiwa mzembe sitampa nafasi ligi ikianza," alisema.

# LYANGA AIFUNGUA MDOMO COASTAL

**Na Saada Akida**

HUKU klabu ya Yanga ikielezwa kugeuzia rada zake kwa nyota wawili wa Coastal Union, uongozi wa klabu hiyo ya jijini Tanga umetoa angalizo kuwa utawachukulia hatua kali wale wote wanaofanya mazungumzo na wachezaji wenye mikataba zaidi ya miezi sita.

Tayari kuna tetesi kwamba uongozi wa Yanga upo katika rada za kuhitaji huduma ya nyota wa Coastal, ambao ni beki Ibrahim Ame na mshambuliaji Ayoub Lyanga.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Coastal Union, Hemed Aurora, alisema nyota hao ni moyo wa timu yao na wana mikataba kuanzia mwaka mmoja wa kuitumikia timu hiyo.

**Alisema milango yao ipo wazi kwa viongozi wa timu inayohitaji mchezaji yeyote kwa kwenda mezani kufanya mazungumzo ya kuipata huduma yake.**

"Hatuwezi kumzuia mchezaji kuondoka, hivyo kama kuna mtu amepata ofa na yupo katika mkataba basi hao viongozi wanatakiwa kufuata kanuni ya usajili kwa wenye mikataba waje tuzungumze na tuafikiane.

"Hao wachezaji wanaotajwa kutakiwa ni moyo wa timu yetu, bado wana mikataba na sisi, hivyo waje kwetu tuzungumze na tuangalie kama kuna maslahi na si kuzunguka kwenda moja kwa moja kwa wachezaji hao," alisema Aurora.

Alisema hawawezi kumbania mchezaji ambaye wana mkataba nae kwenda kuangalia maisha katika klabu nyingine ilhali watapata maslahi kupitia kumuuza nyota husika.

KIVYANGU VYANGU...



Kipa wa Simba na timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Aishi Manula akifanya mazoezi binafsi jijini Dar es Salam wiki iliyopita kujiweka fiti zaidi katika kipindi hiki ambacho klabu yake imesitisha mazoezi ya pamoja kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19). **NA MPIGAPICHA WETU**



## *Azam FC yamulika msimu wa 2020/21*

**Na Saada Akida**

WAKATI hatima ya Ligi Kuu Bara msimu huu ikiwa bado haijajulikana, uongozi wa Azam FC, umesema mpango mkubwa uliopo kwa sasa ni kujenga kikosi imara kwa ajili ya mashindano ya kitaifa na kimataifa kwa msimu ujao wa 2020/21.

Ligi Kuu Bara ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu baada ya serikali kuzuia shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), na hadi sasa haijajulikana ni lini itarejea tena.

Hata hivyo, wakati ikiweka mipango ya msimu ujao kuna taarifa kwamba nyota wa Asante Kotoko, Sogne Yacouba (pichani) kuingia kwenye rada za kutakiwa na Azam kwa ajili ya kuboresha kikosi chao.

Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin, ameliambia gazeti hili jana kwamba bado kuna mipango inaendelea kupangwa na mingine inatimizwa taratibu kufikia malengo.

Alisema mchakato wa usajili wa wachezaji wapya bado haujaanza kutokana na kusubiriwa mapendekezo ya kocha wao, Mromania Aristica Cioaba.

"Kufikia malengo yalipo si safari ya siku moja kuna mchakato ambao tunapitia kwa hatua ambayo tupo ni lazima tuwe na subira," alisema Popat.

Alisema kwa sasa wanahesabu kali kufikia mafanikio kitaifa na kimataifa, huku wakihitaji sapoti ya pamoja kwa lengo la kufikia kile wanachokipanga kwa msimu mpya.

Michezo
Jumatatu Mei 4, 2020
Nipashe



De Bruyne: Fedha zinairudisha EPL UKURASA 22

AMUENI MOJA...



Benchi la ufundi la vinara wa Ligi Kuu Bara, Simba, wanaosikilizia endapo Ligi Kuu Bara itarejea ama la, Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck (kulia) na wasaidizi wake, Selemani Matola na kocha wa makipa, Muharami Mohammed (katikati). **PICHA: MAKTABA**

# MAGUFULI: NAFIKIRIA KURUHUSU LIGI KUU

## ●●● Ni wakati TFF ikijifungia kujadili hatima ya ligi hiyo, asema wanaofanya mazoezi corona...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilitarajia kujifungia kujadili hatima ya ligi kuendelea ama kufutwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli amesema anafikiria kuruhusu ligi za mpira kuendelea na anachosubiri kwa sasa ni wataalamu wake tu kumshauri.

**Machi 17, mwaka huu serikali ilipiga marufuku shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo yote ikiwamo Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili, kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19) na bado haijajulikana ni lini itaruhusiwa tena kurejea.**

Lakini jana akiwa Chato mkoani Geita wakati akimwapisha, Dk. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Marehemu Balozi Dk. Augustine Mahiga, aliyefariki dunia Mei Mosi, mwaka huu, Rais Magufuli alisema wazi kwa siku zinazokuja mbeleni anafikiria kuirejesha ili watu angalau wawe wanaangalia kupitia TV.

"Watanzania tusiwe na hofu, tuendelee kuchapa kazi, wanasiasa waache kutumia hii kama ajenda, haitaweza kuwasaidia, Watanzania lazima tuishi, kwa siku zinazoendelea ninafikiri kuruhusu hata ligi za mipira ziendelee, nasubiri wataalamu wangu wanishauri.

"Na kiukweli siku zinazokuja mbeleni ninafikiria hata kuruhusu ligi iendelee, ili watu wawe wanacheza angalau wanaangalia kwenye TV, tuweke utaratibu mzuri kwa sababu ninaelewa hata kwa walioathirika na corona sijaona mwanamichezo hata mmoja ambaye amedhurika sana kwenye hili.

"Na hii inadhihirisha wazi kuwa kwa wale wanaofanya mazoezi corona inawakwepa sasa kama tunawazuia kucheza maana yake tunawaambia waugue corona," alisema Rais Magufuli.

Tayari wadau wengi wa soka, walishaanza kupaza sauti zao wakitaka ligi hiyo ifutwe na washindi wa msimu uliopita, Simba kwa upande wa Ligi Kuu kuwa mwakilishi wa nchi kwenye Ligi ya Mabingwa, huku Azam FC ambayo ilikuwa bingwa wa FA Cup msimu uliopita, kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hadi Ligi Kuu inasimama, ilibakiza takriban raundi 10 kabla kumalizika huku Simba ikiwa kileleni mwa msimamo na alama 71, ambazo ni 17 mbele ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili huku Yanga ikiwa ni ya tatu na pointi zake 51, lakini ikiwa nyuma kwa mchezo mmoja.

Jana TFF ilitarajiwa kujadili mustakabali wa ligi hiyo kuendelea ama la kutokana na agizo la Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kuwataka wanachama wake wote kutoa hatima ya ligi zao kabla ya kesho Mei 5, mwaka huu ili kuiwezesha kuandaa kalenda zake za michuano mbalimbali.

## Messi, Maradona wachambuliwa

**BUENOS AIRES,** Argentina

DIEGO Maradona alikuwa na "kipaji halisi" na Lionel Messi ana "kasi ya Gonzales", kwa mujibu wa kocha msaidizi wa timu ya Taifa ya Argentina, Roberto Ayala.



HABARI UK. 20

## Aubameyang amtia hofu Adams Arsenal

**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang anatakiwa kuondoka Arsenal wakati wa dirisha la usajili kwa sababu imekuwa klabu ya kuuza wachezaji, nahodha wa zamani wa 'Washikabunduki' hao, Tony Adams amesema.



HABARI UK. 21

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >